**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

# MKAKATI WA TAIFA WA USIMAMIZI WA MAAFA (2022 – 2027)

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

## OFISI YA WAZIRI MKUU

# MKAKATI WA TAIFA WA USIMAMIZI WA MAAFA (2022 – 2027)

**Haki miliki**

© Ofisi ya Waziri Mkuu 2022. Inaruhusiwa kudurufu ili mradi chanzo kitambuliwe.

**Nukuu**

"Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2022). Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa 2022 – 2027. Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Menejimenti ya Maafa.

# YALIYOMO

YALIYOMO ........ I
ORODHA YA MAJEDWALI ........ III
ORODHA YA VIELELEZO ........ IV
MISAMIATI ILIYOTUMIKA ........ V
DIBAJI ........ VII
SHUKRANI ........ XI
MUHTASARI ........ X
SEHEMU YA KWANZA ........ 1
1.0 UTANGULIZI ........ 1
1.1 Chimbuko ........ 1
1.2 Hatari za maafa katika muktadha wa shughuli za maendeleo ........ 2
1.3 Madhumuni na utaratibu wa kuandaa mkakati ........ 2
SEHEMU YA PILI ........ 6
2.0 UCHAMBUZI WA HALI HALISI ........ 6
2.1 Hali ya maafa nchini Tanzania ........ 6
2.2 Hatari za maafa zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi nchini Tanzania .... 13
2.3 Hali ya uwezekano wa kutokea kwa hatari ya maafa nchini Tanzania ........ 17
2.4 Uchambuzi wa uwezo, maeneo ya kuboresha, fursa na changamoto ........ 19
SEHEMU YA TATU ........ 24
3.0 DIRA, DHIMA NA MALENGO ........ 24
3.1 Dira ........ 24
3.2 Dhima ........ 24
3.3 Malengo ........ 24
3.3.1 Lengo kuu ........ 24
3.3.2 Malengo mahususi ........ 24
3.4 Kanuni ongozi za usimamizi wa maafa ........ 25
SEHEMU YA NNE ........ 26
4.0 UTEKELEZAJI WA MKAKATI ........ 26
4.1 Uelewa wa vihatarishi vya maafa ........ 26
4.2 Kuzuia, kupunguza madhara na kujiandaa na maafa ........ 28
4.3 Mfumo changamano wa tahadhari ya mapema ........ 31
4.4 Uwezo wa kukabiliana na maafa na huduma za kibinadamu ........ 32
4.5 Kurejesha hali, kukarabati na kujenga upya kwa ubora zaidi ........ 34
4.6 Rasilimali na uwekezaji katika usimamizi wa maafa kwenye sekta ya umma na binafsi ........ 35
4.7 Mfumo wa utendaji wa usimamizi wa maafa ........ 36
4.8 Jinsia, vijana, watu wenye ulemavu na mahitaji ya makundi maalum mengineyo pamoja na utofauti wa tamaduni ........ 38
4.9 Ushirikiano wa kikanda na kimataifa ........ 39
4.10 Hifadhi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi ........ 41

SEHEMU YA TANO ........ 43
5.0 BANGO KITITA LA UTEKELEZAJI WA MKAKATI ........ 43
SEHEMU YA SITA ........ 86
6.0 MFUMO WA KISERA, KISHERIA NA KITAASISI ........ 86
6.1 Mfumo wa Kisera ........ 86
6.2 Mfumo wa Kisheria ........ 86
6.3 Mfumo wa Kitaasisi ........ 86
6.4 Majukumu na wajibu wa watendaji mbalimbali ........ 91
6.5 Mipango ya kifedha ........ 95
SEHEMU YA SABA ........ 97
7.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI ........ 97
7.1 Utangulizi ........ 97
7.2 Malengo ya mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ........ 98
7.3 Mpangilio wa kitaasisi wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ........ 98
7.4 Viashiria vya ufuatiliaji na tathmini ........ 99
7.5 Zana na matokeo ya ufuatiliaji na tathmini ........ 99
7.6 Taarifa za ufuatiliaji na tathmini ........ 100
REJEA ........ 110

# ORODHA YA MAJEDWALI

JEDWALI NA. 1: UCHAMBUZI WA UWEZO, MAENEO YA KUBORESHA, FURSA NA CHANGAMOTO ................................................ 21

JEDWALI NA. 2: BANGO KITITA LA MKAKATI ............................................ 43

JEDWALI NA. 3: AINA YA TAARIFA ZA UFUATILIAJI NA TATHMINI ..... 100

JEDWALI NA. 4: VIASHIRIA VYA UTENDAJI VYA MFUMO WA .................... UFUATILIAJI NA TATHMINI YA USIMAMIZI WA MAAFA .. 101

# ORODHA YA VIELELEZO

KIELELEZO NA. 1: MCHANGANUO WA MATUKIO, VIFO NA WATU WALIOATHIRIWA (1997-2017) ........................................................................ 4

KIELELEZO NA. 2: MATUKIO YA MAAFA NCHINI (1997 – 2017) ............ 4

KIELELEZO NA. 3: JANGA LA TETEMEKO LA ARDHI NCHINI TANZANIA ............................................................................................................ 7

KIELELEZO NA. 4: IDADI YA WATU WALIOATHIRIWA NA MAFURIKO KWA KIPINDI CHA HALI YA HEWA YA SASA NA MAKADIRIO YA SIKU ZIJAZO .......................................................................... 9

KIELELEZO NA. 5: IDADI YA WATU WALIOATHIRIWA NA UKAME KWA KIPINDI CHA HALI YA HEWA YA SASA NA MAKADIRIO YA SIKU ZIJAZO .......................................................................... 10

KIELELEZO NA. 6: INFORM TANZANIA – KIWANGO CHA HATARI ... 10

KIELELEZO NA. 7: MFUMO WA USIMAMIZI WA MAAFA TANZANIA .. 44

# MISAMIATI ILIYOTUMIKA

| | |
|---|---|
| Afya moja | maana yake ni dhana inayotumika kuweka ushirikiano baina ya sekta zinazohusika na afya ya binadamu, wanyama na mazingira, ili kuimarisha uratibu na usimamizi katika utendaji na kupanga mikakati ya pamoja inayolenga kuzuia, kujiandaa na kukabiliana na milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea na mazao ikiwemo madhara ya majanga yanayovuka mipaka na yanayoweza kusambaa kwa muda mfupi, usugu wa madawa, usalama wa chakula na lishe na magonjwa yasiyo ya kuambukiza. |
| Janga | maana yake ni balaa au baa linalotokana na nguvu za asili au shughuli za kibinadamu ambalo linaweza kusababisha maafa. |
| Kukabiliana na maafa | maana yake ni hatua yoyote inayochukuliwa mara tu baada ya maafa kutokea ili kuokoa maisha, mali na mazingira, kupunguza madhara ya kiafya, kutoa huduma za kibinadamu, kuimarisha usalama wa umma au kushughulikia uharibifu unaotokana na maafa |
| Kupunguza madhara | maana yake ni hatua zinazoelekezwa katika kupunguza madhara ya maafa yanayoweza kusababishwa na tukio la janga. |
| Kurejesha hali baada ya maafa | maana yake ni hatua zinazosaidia kurejesha hali au kuboresha mifumo ya maisha iliyoathiriwa na maafa kwa kujenga upya au kurejesha mifumo kwa ubora zaidi ili kuzuia au kupunguza madhara ya maafa siku zijazo. |
| Kuzuia maafa | maana yake ni hatua zinazochukuliwa kuzuia hatari mpya au kupunguza hatari zilizopo kutokana na shughuli na maamuzi ya kibinadamu au nguvu za asili yasisababishe kutokea kwa maafa. |
| Maafa | maana yake ni madhara yanayotokana na janga ambayo yanajumuisha uharibifu wa mfumo wa kawaida katika jamii, kusababisha vifo, majeruhi, madhara ya kisaikolojia, upotevu au uharibifu wa mali, mifumo mbalimbali ya kiteknolojia na huduma za kiuchumi na kijamii au mazingira kwa kiwango chochote ambapo jamii iliyoathirika haiwezi kukabili kwa kutumia rasilimali zake bila msaada kutoka nje ya jamii hiyo. |

| | |
|---|---|
| Makundi maalum | maana yake ni makundi yanayojumuisha watoto, wanawake wajawazito, wazee, watu wenye ulemavu, watu wenye utapiamlo, wakimbizi, wahamiaji wa ndani na wagonjwa au wenye upungufu wa kinga. |
| Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa | maana yake ni mkakati ambao unaainisha hatua zitakazochukuliwa katika kuzuia na kupunguza madhara ya majanga pamoja na kujiandaa kukabili na kurejesha hali pindi maafa yanapotokea |
| Usimamizi wa maafa | maana yake ni utekelezaji wa sera na mikakati ya kupunguza hatari za maafa ili kuzuia hatari mpya, kupunguza hatari zilizopo na kudhibiti hatari zilizobaki kwa lengo la kuimarisha ustahimilivu na kupunguza hasara za maafa |

# DIBAJI




Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa ni matokeo ya dhamira ya Serikali ya Tanzania kulinda maisha ya watu na mali zao kutokana na madhara ya maafa. Mkakati una lengo la kuwa na jamii yenye ufanisi na uwezo wa kuzingatia vihatarishi na kukabiliana na maafa kwa maendeleo endelevu. Hali hii itafikiwa kupitia uwajibikaji na ushirikiano wa watendaji wote na kuwezesha jamii na taasisi katika kuchukua hatua zinazofaa ili kuzuia na kupunguza madhara ya maafa kwa kibinadamu na mifumo ya maisha yanayosababishwa na matukio ya majanga. Haya yote yanahitaji rasilimali na kujitolea kwa hali ya juu.

Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa upunguzaji wa hatari za maafa unakuwa nguzo na sehemu muhimu ya sera na programu za kitaifa. Tutazingatia mbinu shirikishi katika usimamizi wa maafa na huduma za kibinadamu. Mkakati umeweka msisitizo wa kufanya kazi kwa pamoja na wadau wote ili kuendeleza na kutekeleza ushirikiano wa kimkakati, kisayansi na ubunifu kwa ajili ya jamii stahimilivu.

Mkakati huu umeandaliwa kwa kuelewa kwamba mafanikio na mipango yote ya maendeleo yanahitaji kulindwa dhidi ya madhara ya matukio ya maafa. Hivyo, Mkakati umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025, Mpango Elekezi wa Muda Mrefu (2011/12 – 2025/26), Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na sera, mikakati na mipango mbalimbali ya kisekta. Aidha, Mkakati unawiana na mifumo ya Kikanda na Kimataifa inayohusu usimamizi wa maafa kama vile Mkakati wa Sendai wa kupunguza hatari za Maafa 2015 – 2030, Malengo ya Maendeleo Endelevu, Mkataba wa Paris wa Mabadiliko ya Tabianchi na Mkakati wa Kikanda wa Afrika wa Kupunguza Hatari za Maafa.

Mkakati umeainisha hatua za kuchukua zinazoendana na mipango ya kisekta, programu na mikakati katika kushughulikia hatari za maafa, usimamizi wa huduma za kibinadamu na kutekeleza hatua za kurejesha hali. Hatua hizi zinaonyesha dhamira ya mabadiliko ya mtazamo kutoka kusubiri kukabiliana na maafa kuelekea katika utamaduni wa dhana pana ya kuzuia au kupunguza vihatarishi vya maafa. Nawaomba wadau wote wa usimamizi wa maafa kushiriki

kikamilifu katika utekelezaji wa Mkakati huu muhimu.



Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)

**WAZIRI MKUU**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**


# SHUKRANI



Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa ni matokeo ya juhudi za ushirikiano kutoka kwa wadau mbalimbali nchini, Kikanda na Jumuiya za Kimataifa. Ushiriki wa wadau kutoka ngazi mbalimbali ni muhimu ikizingatiwa kuwa dunia ikiwemo nchi yetu inashuhudia kuongezeka kwa hatari za maafa zinazosambaa kwa haraka na kusababisha madhara yanayohitaji juhudi za pamoja na jumuishi za kuyadhibiti. Hivyo, Mkakati huu utachangia kuimarisha utekelezaji wa hatua shirikishi za kudhibiti majanga, zinazo jumuisha juhudi za Serikali na wadau nje ya Serikali.

Ninashukuru kwa maoni, michango na mapendekezo kutoka Wizara, Idara na Taasisi, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umoja wa Mataifa na Kimataifa, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Taasisi za Dini, Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda, Taasisi za Taaluma na Utafiti, Wanahabari na wadau wengine katika kuandaa mkakati huu. Kipekee, natoa shukrani zangu za dhati kwa Wataalam na Viongozi wa Idara ya Menejimenti ya Maafa kwa juhudi zao za kuratibu na kuandaa Mkakati huu kwa kushauriana na wadau wa usimamizi wa maafa.

Hivyo, Mkakati umezingatia matakwa na nia za wadau wengi wa usimamizi wa maafa kwa kadri inavyowezekana. Natumaini kuwa wadau watatumia Mkakati huu katika kutekeleza shughuli za usimamizi wa maafa katika sekta zao kwa ajili ya kuwa na jamii endelevu na stahimilivu dhidi ya maafa.



Dkt. John A. K. Jingu

**KATIBU MKUU**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**(SERA, BUNGE NA URATIBU)**

# MUHTASARI

Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa umeandaliwa kwa ajili ya kutekelezwa katika kipindi cha 2022 – 2027. Hii inatokana na ukweli kwamba Tanzania itaendelea kuwa katika hatari ya kukumbwa na maafa kutokana na kuwepo kwa viashiria kadhaa ikiwa ni pamoja na mazingira ya kijiografia, mabadiliko ya hali ya hewa, uwekezaji wa baadhi ya rasilimali katika mazingira hatarishi, ongezeko la haraka la watu mijini, kuwepo kwa makazi yasiyopangwa mijini na uharibifu wa mazingira. Matukio ya majanga yaliyosababisha maafa hivi karibuni ni pamoja na matetemeko ya ardhi, mafuriko, magonjwa ya mlipuko, ukame na moto, pamoja na ajali za barabarani, treni na kwenye maji na kukatizwa kwa huduma za TEHAMA ikijumuisha kukatika kwa huduma, udukuzi na uharibifu wa miundombinu kama Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kukabiliana na maafa ikiwa ni pamoja na kuandaa Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa, Mwongozo wa Taifa wa Menejimenti ya Maafa na Sheria ya Usimamizi wa Maafa na kanuni zake. Utekelezaji wa Sera, Sheria na Miongozo mingine imechangia kuimarisha hatua za kupunguza hatari za maafa na utoaji wa huduma za kibinadamu nchini.

Pamoja na mafanikio hayo, kumekuwepo na changamoto kadhaa katika usimamizi wa maafa ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa matukio na kiwango cha madhara ya maafa, uwezekano mkubwa wa kutokea maafa yanayovuka mipaka, uzingatiaji mdogo wa masuala ya usimamizi wa maafa katika mipango ya maendeleo, ushirikishwaji na uelewa mdogo wa wananchi, ukosefu wa mifumo jumuishi ya tahadhari ya mapema na kutotomika kikamilifu taarifa na mifumo ya kijiografia katika usimamizi wa maafa. Miongoni mwa kikwazo cha kukabiliana na changamoto hizi ni ukosefu wa Mkakati madhubuti na jumuishi wa usimamizi wa maafa.

Aidha, kuna maendeleo ambayo yamefanyika katika ngazi ya Kimataifa na Kikanda kuhusu usimamizi wa maafa kama vile Mfumo wa Kupunguza Madhara ya Maafa wa Sendai 2015 - 2030, Mpango wa Utekelezaji wa Kupunguza Madhara ya Maafa 2015 – 2030 barani Afrika, Ajenda ya Maendeleo Endelevu ya 2030, Mkataba wa Makubaliano wa Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi, Ajenda ya Huduma za Kibinadamu ya 2016, Ajenda Mpya kuhusu Miji na Ajenda ya 2063: Afrika Tunayoitaka. Serikali imeweka ahadi kutekeleza Makunaliano ya hiyari na hivyo kuna haja ya kuwa na mikakati

ya utekelezaji wake inayowiana na malengo tarajiwa. Mkakati huu pia unaendana na mikakati mbalimbali ya kitaifa ikiwamo Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025, Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2011/12 – 2025/26, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Sera, Mikakati na Mipango mbalimbali ya kisekta.

Mkakati unatokana na dhamira ya Serikali katika kuchukua hatua za usimamizi wa maafa kwa ajili ya ustahimilivu wa jamii. Msisitizo unawekwa katika kushughulikia hatari za majanga ya aina tofauti tofauti kwa pamoja, ushirikiamo wa sekta mbalimbali, kuzingatia wajibu wa taasisi na kisekta kwa mujibu wa sheria, taratibu, taaluma na nyenzo zilizopo na uwajibikaji wa pamoja kwa jamii nzima katika usimamizi wa maafa kwa ajili ya kufikia maendeleo endelevu. Pia, kuimarisha ushirikiano baina ya hatua zinazochukuliwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kupunguza hatari za maafa na utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu ili kuzuia kutokea kwa hatari mpya na kupunguza hatari zilizopo na za baadaye.

Mkakati huu una malengo kumi ambayo yamejikita katika kushughulikia hatari za maafa na kuimarisha huduma za kibinadamu nchini. Malengo hayo ni pamoja na kuongeza uelewa wa vihatarishi vya maafa katika ngazi zote; kuimarisha uwezo wa kuzuia, kupunguza madhara na kujiandaa na maafa katika ngazi zote kwa ajili ya ustahimilivu wa jamii; kuboresha mifumo changamano ya tahadhari ya mapema ya majanga tofauti tofauti kwa kuzingatia mahitaji ya jamii; kuimarisha uwezo wa kukabiliana na maafa na huduma za kibinadamu katika ngazi zote; na kuongeza uwezo wa kurejesha hali, kukarabati na kujenga upya kwa ubora zaidi kwa ajili ya ustahimilivu wa jamii. Malengo mengine ni kuongeza upatikanaji wa rasilimali na uwekezaji katika usimamizi wa maafa kwenye sekta ya umma na binafsi; kuimarisha mifumo ya utendaji ya usimamizi wa maafa katika ngazi zote; kuimarisha mchangamano wa jinsia, vijana, watu wenye ulemavu na mahitaji ya makundi maalum mengineyo pamoja na utofauti wa tamaduni katika usimamizi wa maafa; kuimarisha utekelezaji wa maazimio ya kikanda na kimataifa ambayo yameridhiwa; na kuimarisha mbinu shirikishi za kisekta katika kudhibiti uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa ajili ya kuhimili maafa.

Utekelezaji wa Mkakati wa utazingatia mfumo wa Kisera, Kisheria na Kitaasisi wa usimamizi wa maafa uliopo. Mfumo umeainisha majukumu ya taasisi na wadau kupitia kamati za usimamizi wa

maafa kuanzia ngazi ya taifa hadi kijiji au mtaa. Taasisi zinazohusika zimeainishwa kwenye bango kitita ambalo linajumuisha malengo, mikakati, shabaha, rasilimali na muda utekelezaji.

Mfumo wa tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati umezingatia na mifumo iliyopo katika Wizara, Idara na Taasisi, Mamlaka za Serikali za Mikoa na Serikali za Mitaa. Orodha ya viashiria imeandaliwa kwa ajili ya kufuatilia maendeleo wa utekelezaji wa Mkakati ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Viashiria hivi vitafanyiwa marejeo kila mwaka ili kupata taarifa za ziada. Takwimu za awali zitakusanywa na kuhuishwa kwa ajili ya kuweka msingi wa kimkakati wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mkakati. Mtiririko wa taarifa katika utekelezaji wa mkakati utazingatia mfumo wa Serikali wa kutoa taarifa uliopo.

# 1.0 UTANGULIZI

## 1.1 Chimbuko

Tanzania inakabiliwa na hatari ya kuathirika kutokana na madhara ya maafa mbalimbali ambayo yanachangiwa zaidi na mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa, uwepo wa rasilimali na ongezeko la watu katika maeneo yaliyo katika mazingira hatarishi, kuwepo kwa makazi yasiyopangwa mijini na uharibifu wa mazingira. Hali hiyo imekuwa na matokeo hasi na hivyo kuathiri maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Matukio ya majanga yaliyosababisha maafa hivi karibuni ni pamoja na tetemeko ya ardhi, mafuriko, magonjwa ya mlipuko kwa binadamu na wanyama, ukame, moto, pamoja na ajali za barabarani, treni na kwenye maji. Matukio haya yamesababisha vifo, uharibifu wa miundombinu na kuathiri mifumo ya maisha na mazingira. Kuendelea kwa matukio haya kumesababisha chanagamoto za kijamii na kiuchumi, kuathiri maendeleo yaliyopatikana kwa miaka mingi na kuongeza uwezekano wa kuathiriwa na majanga na kupunguza uwezo wa kukabiliana na maafa.

Serikali imekuwa ikichukua hatua za kukabiliana na athari za maafa ikiwa ni pamoja na kutunga Sera na Sheria ambazo zinaainisha wajibu wa sekta na taasisi mbalimbali ili kuchukua hatua za usimamizi wa maafa, ufuatiliaji wa mwenendo wa majanga kwa ajili ya tahadhari ya mapema na kutoa misaada ya kibinadamu. Jitihada hizi zinaonekana kutekelezwa tangu mwaka wa 1990 wakati ilipotungwa Sheria ya Uratibu wa Misaada ya Maafa Sura ya 242. Sheria hii ilitoa mamlaka ya uratibu usimamizi wa maafa nchini kwa Ofisi ya Waziri Mkuu na kuanzisha Kamati ya Wizara za Kisekta inayojulikana kama Kamati ya Taifa ya Kuratibu Misaada ya Maafa kusimamia misaada nchini.

Aidha, Serikali ilifuta Sheria ya Uratibu wa Misaada ya Maafa Sura ya 242 na kutunga Sheria ya Usimamizi wa Maafa Sura ya 242. Sheria ya Usimamizi wa Maafa, pamoja na masuala mengine ilianzisha Baraza la Usimamizi wa Maafa Tanzania kuchukua nafasi ya Kamati pamoja na kuanzisha Kamati za Usimamizi wa Maafa kuanzia ngazi ya Mkoa hadi Kijiji. Aidha, ili kuimarisha mfumo wa usimamizi wa maafa nchini, Serikali ilitunga Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 6 ya mwaka 2022 ambayo imezingatia utaratibu wa utendaji uliopo kuanzia ngazi ya taifa mpaka Kijiji au Mtaa. Sheri hii imeanzisha Kamati Elekezi za Usimamizi wa Maafa katika ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya pamoja na Kamati za Wataalam za Usimamizi wa Maafa

katika ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya. Vilevile, Sheria imezingatia uwepo wa Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi ya Kata na Kijiji au Mtaa. Mbali na Sheria hiyo, shughuli za usimamizi wa maafa nchini Tanzania zinatekelezwa kwa kuzingatia Mwongozo wa Taifa wa Operesheni za Maafa wa mwaka 2003 (marejeo ya 2014), Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya mwaka 2004, Mpango wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa wa mwaka 2022, Mkakati wa Mawasiliano Wakati wa Dharura wa mwaka 2022.

Vilevile, zipo Sera na Sheria zinazosaidia usimamizi wa maafa katika Wizara za kisekta na Wakala mbalimbali. Sera na Sheria hizi zinashughulikia masuala mbalimbali yanayohusiana na usimamizi wa maafa ikiwa ni pamoja na mazingira na mabadiliko ya tabianchi, milipuko ya magonjwa kwa binadamu, usalama wa chakula na lishe, mafuriko na uchafuzi wa vyanzo vya maji, milipuko ya magonjwa ya wanyama na wadudu waharibifu, mipango miji, shughuli za uchimbaji madini na msaada wa kijeshi kwa mamlaka za kiraia wakati wa dharura. Nyingine ni pamoja na zinazoelekeza kutoa huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na udhibiti wa moto, utafutaji na uokoaji; tahadhari ya mapema kwa majanga yanayohusiana na hali ya hewa; ulinzi dhidi ya mionzi na usalama dhidi ya nyuklia; misaada ya kibinadamu; udhibiti wa madhara ya kemikali; kuzuia na kudhibiti ajali za baharini na kumwagika kwa mafuta; na usalama wa safari za anga. Aidha, kuna wizara na wakala zenye idara na vitengo pamoja na mikakati na mipango ya kisekta ya usimamizi wa maafa.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kupunguza madhara ya maafa kupitia utekelezaji wa Sera na Sheria hizo nchini, kumekuwepo na ongezeko la matukio ya maafa yenye athari kubwa katika sekta mbalimbali. Hali hii imetokana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza ikiwa ni pamoja na kutozingatia ipasavyo hatari ya maafa katika sera za kisekta, mipango, programu na bajeti; kutotambulika kikamilifu kwa vyanzo vya majanga, sababu za uwezekano wa kusababisha madhara na uwepo wa rasilimali katika mazingira hatarishi; kuongezeka kwa idadi na uwezekano wa hatari za majanga yanayovuka mipaka; kutokuzingatia kikamilifu hatua madhubuti za kushughulikia matukio madogo madogo na ya mara kwa mara ya maafa, tathmini ya uharibifu na mahitaji, tathmini ya hatua zilizochukuliwa kukabiliana na maafa na uratibu wa rasilimali miongoni mwa wadau; kuongezeka kwa majanga na hatari ya maafa kwa sehemu kubwa ya jamii haswa mijini, maeneo ya shughuli nyingi

za kiuchumi na ukanda wa pwani; na kuzingatia udhibiti maafa badala ya hatua kuzuia majanga kutokea na kupunguza madhara ya maafa.

Hivyo basi, ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, Serikali imeandaa Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa (NDMS) kwa ajili ya kutekelezwa katika kipindi cha 2022 – 2027 kwa Tanzania Bara ili kushughulikia vihatarishi na kukabiliana na maafa nchini kwa kushirikisha sekta na wadau wote.

## 1.2 Hatari za maafa katika muktadha wa shughuli za maendeleo

Mkakati umeandaliwa kwa kuzingatia kuwa maendeleo yanahitaji kulindwa dhidi ya madhara ya majanga mbalimbali. Aidha, kwa upande mwingine shughuli za maendeleo zinatakiwa kuzingatia kuzuia na kupunguza madhara ya maafa. Hivyo, Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa 2022 – 2027 unazingatia dhamira ya Serikali ya kuweka mikakati ya kupunguza hatari za maafa na kuimarisha ustahimilivu wa jamii. Mkakati unaendana na mikakati mbalimbali ya kitaifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025, Mpango Mkakati wa Muda Mrefu 2011/12 – 2025/26, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi na sera, mikakati na mipango ya kisekta inayohusiana na usimamizi Maafa. Aidha, Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa unaendana na mifumo ya kikanda na kimataifa ambayo ni pamoja na Mfumo wa Sendai wa Kupunguza Madhara ya Maafa 2015 – 2030, Mpango wa Kupunguza Hatari za Maafa 2015-2030 barani Afrika, Mkakati wa Kupunguza Hatari ya Maafa na Mpango Kazi wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika 2024 – 2030, Makubaliano ya Paris chini ya Mkataba wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi, Ajenda ya Masuala ya Kibinadamu Duniani 2016, Ajenda Mpya ya maeneo ya Mjini na Ajenda 2063: Afrika Tunayoitaka. Mkakati pia unazingatia vipaumbele katika ngazi zote na unatambua umuhimu mkubwa wa masuala yanayoibuka na fursa katika kudhibiti majanga maeneo ya mijini, hali mbaya ya hewa na ushiriki wa sekta binafsi katika kupunguza hatari za maafa. Aidha, mkakati unawiana na Mwongozo wa Kuboresha Upatikanaji, Ufikiaji na Matumizi ya Taarifa za Hatari za Maafa kwa Tahadhari ya Mapema na Hatua za Haraka, iliyoandaliwa kupitia mchakato wa wadau mbalimbali mwaka 2020.[1]

[1] AUC, UNDRR (2020). *Road Map for Improving the Availability, Access and Use of Disaster Risk*

## 1.3 Madhumuni na utaratibu wa kuandaa mkakati

Madhumuni ya mkakati ni kutoa mwongozo wa hatua za kuchukua katika usimamizi wa maafa nchini ili kuimarisha ustahimilivu wa kijamii na kiuchumi na huduma za kibinadamu. Mkakati unazingatia kwa kina usimamizi wa maafa na huduma za kibinadamu kwa njia jumuishi. Pia, unalenga kuimarisha ushirikiano baina ya uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, usimamizi wa maafa na maendeleo endelevu ili kuzuia hatari mapya, kupunguza hatari zilizopo na zinazoweza kutokea miaka ijayo. Mkakati umejikita katika kusimamia majanga tofauti tofauti, ushirikiano wa sekta zote na uwajibikaji wa jamii nzima katika usimamizi wa maafa ili kufikia ustahimilivu kwa maendeleo endelevu katika ngazi zote (ngazi ya taifa hadi kijiji). Kutumia dhana ya majanga mengi katika kuandaa mkakati huu kunachangia kujenga uwezo wa ustahimilivu kwa madhara mbalimbali ya maafa na hivyo kuwa na kiwango cha juu cha ufanisi katika matumizi ya rasilimali.

Hatua za kuandaa mkakati ulihusisha uchambuzi wa taarifa na takwimu za kihistoria za madhara ya maafa na taarifa za tathmini ya hatari za majanga zaidi ya moja na kutathmini uwezo uliopo wa usimamizi wa maafa ikiwemo Sera, Sheria, Mikakati na Mipango na uwekezaji wa rasilimali fedha. Hatua za awali zilihusisha utaratibu wa ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambapo rasimu ya Mkakati iliandaliwa kwa kuzingatia taarifa na takwimu za maafa zilizochambuliwa na taarifa mbalimbali za ndani na nje ya nchi na mifumo ya usimamizi wa maafa. Rasimu ya Mkakati ilijadiliwa na wajumbe wa Jukwaa la Wadau wa Usimamizi wa Maafa ili kupata maoni ya sekta na kujenga umiliki wa pamoja. Ofisi ya Waziri Mkuu ilijumuisha maoni wajumbe wa Jukwaa waliohudhuria na maoni yaliyowasilishwa kwa maandishi kutoka kwa wajumbe ambao hawakuweza kuhudhuria. Aidha, Mkakati uliwasilishwa kwa ajili ya kujadiliwa kwenye Baraza la Usimamizi wa Maafa Tanzania na mapendekezo yao yaliingizwa kwenye katika rasimu. Vilevile, Mkakati uliwasilishwa katika Kikao Kazi cha Makatibu Wakuu ambao walitoa mapendekezo yaliyochangia kuuboresha.

---

*Information for Early Warning and Early Action.* African Union Commission / United Nations Office for Disaster Risk Reduction.


Utekelezaji wa mkakati utahusisha Wizara, Idara na Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi zisizo za Serikali, Mashirika ya Umoja wa Mataifa na Kimataifa, Sekta Binafsi, Wadau wa Maendeleo, Vyombo vya Habari, Taasisi za Elimu, Utafiti na Ufundi na wadau wengine katika usimamizi wa maafa. Rasilimali za utekelezaji wa Mkakati zinajumuisha bajeti ya serikali, fedha za wafadhili na michango kutoka kwa washirika binafsi na jamii. Wadau wa maafa wanatarajiwa kutumia Mkakati kuandaa miradi, program na mipango kazi kwa ajili ya utekelezaji katika sekta zao.

# 2.0 UCHAMBUZI WA HALI HALISI

## 2.1 Hali ya maafa nchini Tanzania

Takwimu kutoka katika kanzidata ya *EM-DAT* zinaonyesha kuwa majanga makuu ya asili yaliyosababisha maafa katika miongo miwili iliyopita (1997 – 2017) ni mafuriko (40%), magonjwa ya mlipuko (34%), tetemeko la ardhi (9%), ukame (6%) na mvua zinazoambatana na upepo mkali (6%). Magonjwa ya mlipuko yamesababisha idadi kubwa zaidi ya vifo (92% ya jumla ya vifo vya maafa). Ukame, kwa upande mwingine, umekuwa ukisababisha madhara kwa idadi kubwa ya watu. Katika miongo miwili iliyopita katika hali ambapo watu walihitaji msaada wa haraka, 91% ilitokana na ukame (Kielelezo 1).


**KIELELEZO NA. 1: MCHANGANUO WA MATUKIO, VIFO NA WATU WALIOATHIRIWA (1997-2017)**




**Chanzo:** *EM-DAT*: Kanzidata ya Matukio ya Maafa – *Université Catholique de Louvain – CRED, 2018*

Takwimu za madhara ya majanga zilizopo katika kanzidata ya Taifa, ambazo zinazokusanywa na kusimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Menejimenti ya Maafa zinaonyesha ongezeko dogo la matukio ya maafa kwa majanga yote yaliyotokea na kuhesabiwa katika miaka kadhaa iliyopita (Kielelezo 2).

**KIELELEZO NA. 2: MATUKIO YA MAAFA NCHINI (1997 – 2017)**




Chanzo: UNDRR (2018), Kanzidata ya takwimu za madhara ya maafa ya DesInventar.

Maelezo ya matuko ya majanga pamoja na takwimu za madhara ya maafa yaliyotokea katika maeneo yaliyoathirika ni kama ifuatavyo: -

Mafuriko yametokea katika Halmashauri mbalimbali nchini, ambapo kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020 yamesababisha vifo vya watu 307, yameathiri watu 317,907 na kuharibu nyumba 50,588. Mikoa ambayo mara nyingi huathiriwa na mafuriko ni pamoja na Dar es Salaam, Tanga, Mwanza, Morogoro, Lindi, Mtwara, Iringa, Dodoma, Kigoma, Rukwa, Pwani na Kilimanjaro. Aidha, mvua ya barafu iliyonyesha wilayani Kahama mwaka 2015 ilisababisha vifo vya watu 47, kuathiri watu 3,500 na kuharibu nyumba 634. El Niño ya mwaka 2015/16 iliathiri moja kwa moja watu 84,643 na kuharibu nyumba 1,006 na hekta 11,167.4 za mazao ya chakula. Pia, iliharibu shule, vituo vya afya, barabara, madaraja, miundombinu mingine ya umma na binafsi katika mikoa ya Mwanza (Ilemela), Mtwara (Mtwara Mikindani na Vijijini), Pwani (Rufiji) na Iringa (Manispaa ya Iringa). Mafuriko mengine makubwa yalitokea mwaka 2009/2010 katika Halmashauri ya wilaya ya Kilosa ambapo watu 2 walifariki na kuathiri watu 26,000. Tukio hili la mafuriko pia liliathiri watu 19,000 katika wilaya za Kongwa na Mpwapwa mkoani Dodoma, kuharibu miundombinu ikiwemo barabara, reli na madaraja na kuchafua vyanzo vya maji. Pia, mafuriko yaliyotokea Jijini Dar es Salaam mnamo mwezi Desemba 2011 yalisababisha vifo vya watu 41, watu

5,000 kupoteza makazi na kuathiri watu 50,000.

Kimbunga cha kitropiki kinachoelekea moja kwa moja kwenye Ukanda wa Pwani wa Tanzania kimekuwa nadra hadi katika miaka ya hivi karibuni ambapo Kimbunga cha kitropiki *Jobo* kilipotokea mwaka 2021 Kaskazini mwa Madagaska na kimbunga cha Tropiki *Kenneth* ambacho kilitua Kaskazini mwa Msumbiji karibu sana na mwambao wa Tanzania mwaka 2019. Baada ya kutokea kwa kimbunga Jobo, kilihamisha mwelekeo kwenda Magharibi-Kaskazini-Magharibi na kutishia kutua nchini Tanzania karibu na Pwani ya Kisiwa cha Mafia tarehe 25 Aprili, kama dhoruba dhaifu ya wastani yenye upepo wa kilomita 45 hadi 80 kwa saa na hivyo kuathiri shughuli za usafiri wa baharini. Kimbunga cha Tropiki Jobo pia kilisababisha ongezeko la mvua zilizoimarishwa katika bonde la Ziwa Victoria nchini Tanzania. Mvua kubwa ilinyesha hadi milimita 59 ndani ya masaa 24 ambayo ni juu ya wastani wa mvua kwa siku katika Ziwa Victoria. Mvua hizi zilisababisha mafuriko ya maji ya Ziwa hivyo kuathiri mfumo wa maisha ya jamii na mazingira karibu na ziwa hilo. Aidha, kumbukumbu zinathibitisha vimbunga viwili vya kitropiki ambavyo ni adimu vilivyotokea Zanzibar na Bagamoyo mwaka 1872 na Kimbunga cha Lindi mwaka 1952.

Hali ya ukame inaonekana mara kwa mara katika maeneo ya Mikoa ya Kaskazini na Kati ikiwa ni pamoja na Arusha, Manyara, Shinyanga, Simiyu, na Dodoma. Ukame wa hivi karibuni uliotokea kati ya Septemba 2021 na Januari 2024 katika Mikoa ya Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara uliathiri uzalishaji wa mazao, kupungua kwa upatikanaji wa maji na malisho ya mifugo. Hali hii, ilisababisha vifo vya ng'ombe 157,695, mbuzi 48,290, kondoo 94,230, punda 6,135 na ngamia 8. Ukame mkali katika mikoa ya Arusha na Manyara mwaka 2008/2009 ulisababisha vifo vya ng'ombe 56,585, mbuzi 39,766 na kondoo 28,883 wilayani Monduli na ng'ombe 231,832, mbuzi 171,435 na kondoo 92,235 wilayani Longido. Aidha, Matukio ya ukame yaliyotokea wilayani Bahi mkoani Dodoma mwaka 2005/2006 yalisababisha vifo vya ng'ombe 4,871, mbuzi na kondoo 1,974. Ukame ndio sababu kubwa ya uhaba wa maji na chakula na pia unazorotesha maendeleo ya kilimo. Mabadiliko ya hali ya hewa na uharibifu wa mazingira husababisha uwezekano mkubwa wa kutokea kwa ukame na madhara makubwa kwani idadi kubwa ya jamii hutegemea mvua kwa ajili ya kilimo kwa shughuli za kiuchumi.


Magonjwa ya mlipuko ya wanadamu yanaleta wasiwasi mkubwa kutokana na uwezekano wa kusababisha madhara ya kiafya na vifo. Mlipuko wa kipindupindu uliodumu kwa muda mrefu zaidi ulioanza Agosti 2015 hadi Disemba 2018 ulisababisha vifo vya watu 550 na kuathiri watu 33,319 katika wilaya 129. Magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu, homa sugu ya ini na magonjwa mapya yanayoibuka na kujitokeza mara nyingi kama vile homa ya *Dengue*, UVIKO-19 na Chikungunya yana hatari kubwa kwa maisha ya binadamu na uchumi. Ugonjwa wa mlipuko una uwezo wa kuenea haraka. Kwa hivyo, ikiwa hakuna hatua zitakazowekwa kudhibiti kuenea, sekta za afya, jamii na uchumi zitaathirika kwa kiasi kikubwa.

Magonjwa ya wanyama (yanayovuka mipaka na kuathiri binadamu na wanyama) yanazuia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya sekta ya mifugo na pia huwaweka wazalishaji kwenye hatari kubwa na kutokuwa na uhakika wa mfumo wa maisha. Ugonjwa wa Kimeta uliripotiwa wilayani Kiteto mwezi Aprili, 2018 ambapo watu 8 walifariki na kaya 62 kuathirika kwa kula nyama iliyoambukizwa. Mlipuko huo pia ulitokea wilayani Moshi mwezi Februari, 2019 na kuua watu 2.

Milipuko ya wadudu waharibifu ndio kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya sekta ya kilimo nchini Tanzania ambapo inaweza kusababisha hasara kubwa ya mazao ikiwa haitasimamiwa vyema. Uvamizi wa Nzige wa Jangwani katika kipindi cha Januari hadi Machi 2021 uliathiri jumla ya Wilaya tano ambazo ni Mwanga na Siha (Kilimanjaro), Simanjiro (Manyara); na Longido na Monduli (Arusha). Ufuatiliaji ulifanyika na kubaini uwepo wa Nzige katika makundi ya wastani wa milioni 55 katika eneo la nusu kilomita za mraba. Uvamizi wa viwavi jeshi mwaka 2017 uliathiri zaidi mazao ya nafaka hususan mahindi na mpunga katika mikoa ya Geita, Rukwa, Kagera, Pwani, Simiyu, Mwanza, Morogoro, Kilimanjaro, na Njombe. Hasara zilizotokea zinahusishwa na ulinzi duni dhidi ya wadudu na magonjwa vamizi, pamoja na taratibu na teknolojia duni za utunzaji wa mazao baada ya kuvuna.

Uchambuzi wa matetemeko ya ardhi kwa maeneo ambayo yapo ndani ya Mfumo wa Bonde la Ufa wa Afrika Mashariki nchini Tanzania ambayo yapo katika ukanda wa shughuli za miamba na hivyo kuelezwa kuwa katika hatari ya kuathirika kutokana na madhara madogo hadi wastani lakini yenye uwezekano wa kuleta hatari kubwa. Kielelezo Na. 3 kinaonyesha mgawanyo wa kijiografia wa kasi ya juu zaidi ya kuyumba ardhi ambayo inaweza kutokea wakati wa tetemeko la ardhi katika eneo nchini.

## KIELELEZO NA. 3: JANGA LA TETEMEKO LA ARDHI NCHINI TANZANIA[2]




**Chanzo:** *Global Earthquake Model Foundation and the METEOR Project Consortium, 2019*

Tukio la tetemeko la ardhi lililotokea mwaka 2017 huko Mwanza liliua mtu 1 na kujeruhi watu 2 na kuharibu baadhi ya majengo katika shule 4. Tetemeko kubwa la ardhi lililotokea mkoani Kagera Septemba 2016 (ukubwa wa 5.9) lilisababisha vifo kwa watu 17, kujeruhi watu 440, kuathiri 117,721, kuharibu nyumba 2,072 na majengo ya umma 2,191.

Matetemeko ya ardhi yalitokea Sumbawanga Machi 2019, (ukubwa wa 5.5), Mkoa wa Mwanza mwezi Mei, 2017 (ukubwa wa 5.0), Ziwa Natron Julai 2007 (ukubwa wa 5.9), Ziwa Tanganyika Desemba 2005 (ukubwa 6.8) na Kaskazini mwa Dodoma Julai 2002 (ukubwa 5.6). Aidha, tetemeko la ardhi lililotokea Bariadi mwezi Mei 2002 lilisababisha vifo 2 na kujeruhi watu 5, kubomoa nyumba 690 na

[2] The map depicts the geographic distribution of the Peak Ground Acceleration (PGA) with a 10% probability of being exceeded in 50 years, computed for reference rock conditions (shear wave velocity, Vs30, of 760-800 m/s).

kuharibu nyumba 636. Tetemeko hilo la ardhi pia liliharibu baadhi ya majengo katika shule 2 wilayani humo.

Maporomoko ya ardhi hutokea wakati nguvu ya mvuto inayofanya kazi kuimarisha miamba katika mteremko inashindwa na nguvu nyingine na kukatika. Maporomoko ya ardhi yalitokea mwaka 2009 huko Same yalisababisha vifo vya watu 24 na kuua ng'ombe 60, kuharibu kilomita 15 za barabara na mabwawa 15 ya umwagiliaji kutokana na athari ya tope. Matukio ya maporomoko ya ardhi pia yalitokea katika Wilaya ya Makete mwaka 2010 ambayo yalifunga barabara ya kwenda Njombe kwa siku kadhaa. Matukio ya maporomoko ya ardhi yalitokea katika Manispaa ya Arusha Aprili 2019 ambapo watu 3 walifariki dunia na 2 kujeruhiwa; na Wilaya ya Mbogwe mnamo mwezi Oktoba 2019 ambapo watu 2 walifariki. Tukio lingine la maporomoko ya ardhi lilitokea Wilayani Ludewa mwezi Machi 2020 ambapo watu 2 walifariki dunia, watu 5 kujeruhiwa na nyumba 13 kuharibiwa. Matukio mengine ya maafa ya kijiografia yalihusisha mlipuko wa mara kwa mara wa Volkano katika vilima vya Oldonyo Lengai mnamo mwaka 1880, 1917, 1921, 1940, 1966, 1967, 2007 na 2008 ambapo watu, mifugo na mazingira yaliathiriwa.

Moto mijini ni moja ya majanga yanayotokea mara kwa mara nchini hasa katika makazi. Kuna sababu nyingi za kutokea moto mijini ikiwa ni pamoja na matumizi makubwa ya vifaa vya umeme kutokana na ukuaji wa haraka wa miji na ongezeko la watu. Mfululizo wa matukio ya moto shuleni kuanzia mwaka 2016 hadi 2020 umesababisha uharibifu katika baadhi ya majengo katika shule 34 za msingi na sekondari. Aidha, moto uliozuka katika soko la Samunge lililopo Manispaa ya Arusha mwezi Machi 2020 uliteketeza eneo la ekari 3.8 lililokuwa na biashara na miundombinu mbalimbali. Vilevile, mlipuko wa lori la mafuta katika Manispaa ya Morogoro mwaka 2019 uliua watu 105.

Matukio makubwa ya ajali za baharini yaliyotokea yanahusisha Kivuko cha Mv Nyerere kupinduka katika Ziwa Victoria Septemba 2018 na kusababisha vifo vya watu 227 na kujeruhi watu 41. Meli ya Mv Skagit iliyopinduka katika Bahari ya Hindi Julai 2012 na kuua watu 144; Meli ya Mv Spice Islander ilipinduka katika bahari ya Hindi Oktoba 2011 na kusababisha vifo vya watu 203 na 1,370 kupotea; na kivuko cha Ulanga kupinduka katika mto Kilombero Novemba, 2002 na kusababisha vifo vya watu 13 na 6 kupotea. Pia, katika Ziwa

Tanganyika, boti mbili ziligongana Novemba, 2001 na kusababisha vifo vya watu 20 na meli ya MV Bukoba kupinduka katika Ziwa Victoria Mei 1996 na kusababisha vifo vya watu 833.

Ajali katika mgodi wa Nyamalinde mkoani Geita Mei 2017 iliua watu 4 na kujeruhi 3. Pia, ajali ya machimbo ya madini ya Mgodi wa Mgusu, Geita mwezi Machi 2009 iliyosababisha vifo vya watu 7 na majeruhi 3. Aidha, ajali katika Migodi ya Mererani, Arusha Machi 2008 iliyosababisha vifo vya watu 74 na tukio lingine Juni, 2002 lililosababisha vifo vya watu 39 na 3 hawakuonekana. Tukio jingine la ajali lilihusisha treni lilitokea Juni 2002 katika kijiji cha Msangali, Dodoma na kusababisha vifo vya watu 283 na kujeruhi watu 466.


Aidha, kwa mujibu wa Utafiti wa Hali ya Lishe Kitaifa wa mwaka 2018, utapiamlo unaathiri zaidi ya watoto 500,000, kati yao 90,000 wameathiriwa na Utapiamlo Mkali, hali inayoongeza hatari ya magonjwa na vifo vya watoto wakati wa dharura. Ujauzito wa chini kutokana na lishe kabla na wakati wa ujauzito ni moja ya sababu kubwa zinazochangia watoto wenye uzito mdogo. Nchini kote, 7.3% ya wanawake wasio wajawazito wenye umri wa kati ya miaka 15-49 walikuwa na uzito mdogo (BMI<18.5). Hivyo, afua za lishe zinapaswa kuzingatiwa katika usimamizi wa maafa kwa lengo la kupunguza hatari kubwa ya watoto kufariki endapo hawatapata uangalizi unaofaa. Kwa kuzingatia matokeo ya tafiti za hivi karibuni, Mikoa ya Singida, Kigoma, Shinyanga na Simiyu iko kwenye hatari zaidi ya kupata madhara ya utapiamlo.

### 2.2 Hatari za maafa zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi nchini Tanzania


Madhara ya mafuriko na ukame yanaweza kuongezeka kwa kipindi cha hali ya hewa ya sasa na mwenendo wa baadaye. Uchumi wa Tanzania na idadi ya watu wapo katika maeneo yanayokabiliwa uwezekano wa kupata madhara makubwa ya mafuriko. Katika hali ya hewa ya sasa, Pato la Taifa la kila mwaka linalozalishwa katika maeneo yaliyoathiriwa na mafuriko ni wastani wa 0.26% ya jumla ($147 milioni/Y). Katika makadirio ya kipindi kijacho cha hali ya hewa thamani hii inatarajiwa kuongezeka hadi 0.36% (208 milioni$/Y)[3]. Inakadiriwa kuwa idadi ya watu wanaoathirika na mafuriko, kwa wastani karibu 45,000 kila mwaka, inaweza kuongezeka mara nne, na

kufikia 210,000 kila mwaka kwa wastani, kuzingatia hali ya hewa ya baadaye na maendeleo ya kijamii na kiuchumi na hivyo kubadilisha mchanganuo wa mwenendo ya kipato na uwezekano wa kuathiriwa kama inavyoonyeshwa kwenye Kielelezo Na. 4 (PMO, UNDRR na CIMA, 2019).

**KIELELEZO NA. 4: IDADI YA WATU WALIOATHIRIWA NA MAFURIKO KWA KIPINDI CHA HALI YA HEWA YA SASA NA MAKADIRIO YA SIKU ZIJAZO**




**Hali ya hewa ya sasa (1979 - 2018)**




**Makadirio ya kipindi kijacho ya tabianchi na shghughuli za kiuchumi na kijamii (2051 - 2100)**

**Chanzo: PMO, UNDRR and CIMA, 2019**


Idadi kubwa ya watu walioathiriwa wako katikati ya nchi, kutoka magharibi hadi mashariki, hasa katika maeneo ya pwani. Katika siku zijazo, hali hii itakuwa na ongezeko kubwa katika maeneo ya mwisho ya mashariki na magharibi mwa nchi na pia karibu na eneo la Ziwa Victoria. Sekta zinazoathirika zaidi, kwa upande wa hasara za moja kwa moja za kiuchumi, ni sekta ya huduma na kilimo, ikifuatiwa na sekta ya usafirishaji. Mgawanyo wa wastani wa hasara kwa mwaka unafanana sana kwa sekta zote tatu na Mikoa inayoathirika zaidi ni Morogoro, Tanga na Pwani. Madhara makubwa pia yanatarajiwa katika eneo la magharibi ya nchi kwa sekta ya uchukuzi. Hasara za moja kwa moja za kiuchumi zinakadiriwa kuongezeka kwa sekta zote chini ya makadirio ya hali ya hewa ya kipindi kijacho. Sekta ya kilimo pekee ndiyo yenye kupungua kwa makadirio ya hasara inayokadiriwa katika eneo la magharibi (PMO, UNDRR na CIMA, 2019).

Kuna uwezekano mkubwa wa ukame mkali zaidi na wa mara kwa mara kwenye shughuli za kilimo katika hali ya hewa ya baadaye (2051 - 2100). Mahesabu yanaonyesha kuwa kati ya watu milioni 11.8 (kwa wastani, kwa mwaka) wanaoishi katika maeneo yaliyoathiriwa na ukame chini ya hali ya hewa ya sasa, wastani wa watu milioni


4.8 kwa mwaka wanakadiriwa kuathiriwa moja kwa moja. Idadi hii itaongezeka hadi milioni 7.8 chini ya makadirio ya hali ya hewa ya baadaye na inaweza kuongezeka hadi milioni 12 kwa kuzingatia hali ya hewa inayotarajiwa na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi kama inavyoonyeshwa kwenye Kielelezo Na. 5 (PMO, UNDRR na CIMA, 2019).

[4] Hali ya hewa ya sasa inamaanisha mwaka 1951-2000; na hali ya hewa ya baadaye ina maanisha mwaka 2050-2100.

**KIELELEZO NA. 5: IDADI YA WATU WALIOATHIRIWA NA UKAME KWA KIPINDI CHA HALI YA HEWA YA SASA NA MAKADIRIO YA SIKU ZIJAZO**




**Hali ya hewa ya sasa (1979 - 2018)**




**Makadirio ya kipindi kijacho ya tabianchi na shgughuli za kiuchumi na kijamii (2051 - 2100)**

**Chanzo: PMO, UNDRR and CIMA, 2019**


Wastani wa hasara za kiuchumi za kila mwaka katika kilimo kutokana na ukame inakadiriwa kuwa takribani dola milioni 140 chini ya hali ya hewa ya sasa. Takwimu hizi zitaongezeka zaidi ya ya mara mbili kwa makadirio ya hali ya hewa katika kipindi kijacho, ikiwa hakuna hatua za kuhimili mabadiliko ya tabianchi zilizochukuliwa (PMO, UNDRR na CIMA, 2019).

## 2.3 Hali ya uwezekano wa kutokea kwa hatari ya maafa nchini Tanzania

Mfumo wa *INFORM* unaonesha kuwa Tanzania iko katika hatari ya kuathirika na majanga mbalimbali pamoja na uwezo usiokidhi wa kukabiliana nayo. Mwenendo katika miaka mitatu (2018 – 2020) kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo Na. 6 kuna ongezeko la uwezekano wa kuathirika wakati hali ya majanga na uwepo wa rasilimali katika maeneo hatarishi ikisalia kwa  kiwango kilichopo pamoja na uwezo usiokidhi wa kukabiliana nayo.

## KIELELEZO NA. 6: INFORM[4] TANZANIA – KIWANGO CHA HATARI

| | Kiwango | Nafasi | Mwenendo wa miaka 3 |
|---|---|---|---|
| Hali ya Vihatarishi | 5.1 | 41 | → |
| Janga na uwepo wa rasilimali eneo hatarishi | 3.7 | 77 | → |
| Uwezekano wa kuathirika | 5.7 | 32 | ↑ |
| Upungufu wa uwezo wa kukabili | 6.2 | 41 | → |




**Chanzo:** *INFORM, 2021*

Tanzania ipo katika nafasi ya 51 kati ya nchi 180 kwenye orodha ya hali ya hatari ya kuathirika na majanga ya asili duniani. Aidha, ukuaji wa uchumi usiobadilika wa kila mwaka hautoshi kupunguza umaskini ipasavyo ambao unaongeza zaidi uwezekano wa watu kuathirika na hatari ya maafa. Kwa kuwa na jumla ya idadi ya watu takriban milioni 57, na kiwango cha ukuaji wa idadi ya watu cha karibu asilimia tatu, ambapo chini ya 30% ya watu wanaishi chini ya wastani wa umaskini wa kimataifa na karibu asilimia 66.9 ya watu wanajishugulisha katika sekta ya kilimo na mifumo mingine maisha ya kiuchumi inayotegemea hali ya hewa. Hali hiyo inawafanya wananchi wa Tanzania kukabiliwa na uwezekano mkubwa wa matukio yasiyo ya kawaida ya majanga ya asili na mabadiliko ya tabianchi. Tanzania imekuwa ikiathiriwa zaidi na ukame na kuongezeka kwa kina cha bahari (UNU-EHS World Risk Report, 2019).

Licha ya kuwa miongoni mwa nchi zilizo hatarini zaidi na zenye uwezo usiokidhi kuhimilia mabadiliko ya tabianchi, Tanzania pia ni mojawapo ya nchi ambazo hazijaandaliwa vya kutosha kwa mujibu wa *Notre Dame-Global Adaptation Index* (ND-GAIN). Tanzania ipo katika nafasi ya 150 kati ya nchi 181 kutokana na uwezekano mkubwa wa kuathiriwa na mabadiliko ys tsbisnchi (2016). Nchi ya Tanzania imeorodheshwa ya 155 kati ya nchi 180 katika uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Ina uwezo mdogo wa kuboresha na kubadilisha uwekezaji kukidhi hatua za kuhimili mabadiliko ya tabianchi, kama inavyothibitishwa katika nafasi ya 143 kati ya nchi

[4] INFORM ni mfumo unaotathmini mwenendo wa uwezekano wa kutokea kwa madhara ya maafa (global, open-source risk assessment for humanitarian crises and disasters. INFORM is a collaboration between the Inter-Agency Standing Committee Task Team for Preparedness and Resilience and the European Commission)

191 zilizofanyiwa tathmini ya utayari.

Usalama wa chakula na lishe, katika hali ya uwepo, upatikanaji na matumizi, unategemea sana hali ya hewa nchini Tanzania. Kwa hivyo, mabadiliko ya tabianchi yana athari kubwa katika kuongeza umaskini ambao mara nyingi huchochewa na ukosefu wa usawa, hususan katika maeneo ya vijijini. Hii ni pamoja na kukosekana kwa usawa wa kijinsia kwani mara nyingi wanawake na wasichana wa vijijini ni maskini zaidi, wana elimu ndogo na wametengwa katika maamuzi ya kisiasa, kijamii na kaya, na wana njia chache na duni za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Uzoefu wa mvua zisizotabirika, vipindi vya ukame wa muda mrefu na mabadiliko katika maeneo ya ikolojia ya kilimo sio tu yanazidisha umaskini lakini pia yanasababisha kuongezeka kwa maambukizi ya malaria (USAID, 2013). Ripoti ya Tathmini ya Tano (2014) ya Jopo la Wataalam kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi inakadiria kuwa mabadiliko ya hali ya hewa yanaweza kuongeza umaskini na uwezekano wa kuathiriwa na majanga yanazohusiana na hali ya hewa.

## 2.4 Uchambuzi wa uwezo, maeneo ya kuboresha, fursa na changamoto

Uchambuzi umefanyika ili kuainisha uwezo, maeneo ya kuboresha, fursa na changamoto kama msingi wa kuandaa malengo ya mkakati huu katika muktadha wa hatari za maafa katika hali ya kiuchumi, kijamii, kimazingira, kisiasa na kiutamaduni ili kuimarisha ustahimilivu nchini. Kuna uwezo na fursa za kuendeleza ili kuimarisha masuala ya usimamizi wa maafa. Pia, kuna maeneo yanayohitaji kuboreshwa ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika usimamizi wa maafa. Uchambuzi unatokana na matokeo ya warsha mbalimbali, mikutano na mapitio ya nyaraka, na unalenga kupata muhtasari wa hatari za maafa zinazoikabili Tanzania, na kutoa picha ya uwezo wa sasa wa usimamizi wa maafa. Matokeo ya uchambuzi huu ni muhtasari wa jumla wa hali ilivyo katika sekta mbalimbali iliyowezesha kubaini uwezo, maeneo ya kuboresha, fursa na changamoto ambao umetumika kutoa mwelekeo wa kupata malengo kumi ya utekelezaji katika mkakati huu. Uchambuzi wa huo umeoneshwa katika Jedwali Na. 1.

Vyanzo vya taarifa za uchambuzi huu ni ritaarifa mbalimbali za kisekta kuhusu usimamizi wa maafa, Taarifa za Baraza la Usimamizi

wa Maafa Tanzania na Jukwaa la Wadau la Taifa la Usimamizi wa Maafa kuanzia 2017 – 2020, kukutana na Kamati za Usimamizi wa Maafa za Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Morogoro, Mara, Rukwa na Mtwara kati ya mwaka 2018 – 2020, warsha ya Waratibu wa Maafa wa Mikoa na Wilaya kutoka katika Mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam na Dodoma mwaka 2019, taarifa za usimamizi wa maafa kutoka wilaya mbalimbali kwa kipindi cha mwaka 2017 hadi 2020.

Pia imezingatia mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Maafa Sura ya 242 na Kanuni zake za mwaka 2017, Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya mwaka 2004, Muongozo ya Taifa wa Operesheni za Usimamizi wa Maafa wa mwaka 2014, Taarifa ya Tathmini ya Vihatarishi vya Maafa ya mwaka 2001 na 2003 na Tathmini ya Uwezo wa Kukabiliana na Maafa Tanzania Bara ya mwaka 2008, Profaili ya Maafa - Mafuriko na Ukame ya mwaka 2019, Tathmnini ya Bajeti katika kuzingatia afua za Hatari ya Maafa wa mwaka 2020, Uchambuzi wa Faida za Uwekezaji katika Kupunguza Hatari ya Maafa na kujenga Ustahimilivu dhidi ya mafuriko na ukame nchini Tanzania wa 2020, Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025, Mpango wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2011 – 2027 na Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano. Uchambuzi unazingatia hatari za maafa, hali ya uwezekano wa madhara kutokea na uwezo uliopo kwa ajili ya usimamizi wa majanga mbalimbali nchini ambayo yanalazimu utekelezaji wa malengo yote kumi yaliyoainishwa.

**JEDWALI NA. 1: UCHAMBUZI WA UWEZO, MAENEO YA KUBORESHA, FURSA NA CHANGAMOTO**

| MAZINGIRA YA NDANI | |
|---|---|
| **Uwezo** | **Maeneo ya kuboresha** |
| • Kuwepo kwa mfumo wa kitaasisi wa uratibu, idara na wakala zinazoshughulikia maafa.<br>• Kuwepo kwa nyaraka mbalimbali za kutoa miongozo ya usimamizi wa maafa nchini.<br>• Mipango ya kitaifa na kisekta, mikakati na sera inazingatia upunguzaji wa hatari za maafa kwa maendeleo endelevu.<br>• Uwepo wa Vituo vya Operesheni za Dharura vya Kitaifa na Kisekta.<br>• Mfumo wa tahadhari ya awali kwa hali mbaya ya hewa, usalama wa chakula, magonjwa ya milipuko ya binadamu na wanyama.<br>• Uwepo wa maghala yaliyohifadhi misaada ya kibinadamu na akiba ya chakula yaliyowekwa kamkakati kikanda. | • Mfumo wa uendeshaji na kitaasisi wa usimamizi wa maafa.<br>• Uwezo katika masuala ya vifaa, fedha na rasilimali watu.<br>• Kuongeza aina za vifaa vya msaada na akiba ya chakula<br>• Mfumo wa utoaji wa taarifa za tahadhari ya awali unaozingatia mfumo wa uchambuzi wa athari, ushirikiano wa wadau na usambazaji wa taarifa.<br>• Tathmini ya kina ya hatari ya maafa mbalimbali.<br>• Upatikanaji wa takwimu za moja kwa moja ikijumuisha takwimu za anga za eneo husika kama vile Mfumo wa Taarifa za Kijiografia kwenye kupunguza hatari ya maafa. |

| MAZINGIRA YA NJE | |
|---|---|
| **Fursa** | **Changamoto** |
| • Matukio madogo ya maafa yenye madhara madogo ambayo mara nyingi yanatabirika kuzingatia muda na eneo husika.<br>• Utoaji wa mafunzo ya usimamizi ya maafa katika taasisi za elimu.<br>• Mwamko wa vyombo vya habari na jamii katika kukabiliana na maafa.<br>• Utashi wa kisiasa na utayari wa sekta binafsi na wafadhili katika suala la usimamizi wa maafa.<br>• Kuanzisha Kituo cha Usimamizi wa Maafa nchini na idara katika Wizara na Taasisi za Umma. | • Utambuzi na tathmini ya hatari haujatumika vya kutosha na usambazaji hafifu wa taarifa za hatari ya maafa kwa ajili ya mahitaji ya kupunguza hatari ya maafa katika ngazi zote.<br>• Uwezekano mkubwa wa kutokea maafa yanayokuvuka mipaka kama vile magonjwa ya mlipuko, ukame na mafuriko.<br>• Tathmini chache za uharibifu na mahitaji baada ya maafa na uratibu miongoni mwa wadau husika.<br>• Kiwango kikubwa cha mazingira hatarishi katika jamii hasa katika miji na maeneo yenye shughuli za kiuchumi.<br>• Kuzingatia zaidi hatua za kukabili maafa badala ya kuwekeza katika kuzuia na kupunguza hatari ya maafa katika ngazi zote. |

Uchambuzi wa uwezo, maeneo ya kuboresha, fursa na changamoto unatoa njia zinazofaa na hatua madhubuti za kupunguza na kudhibiti hatari za maafa ili kuokoa maisha, na kulinda mazingira na uchumi kwa sasa na siku zijazo. Ili kufikia azma hiyo, mkakati unaainisha malengo kumi ya kupunguza hatari ya maafa na huduma za kutoa huduma za kibinadamu. Aidha, utatoa mwongozo wa hatua za kuchukuliwa na watendaji mbalimbali ili kutambua na kukabiliana na hatari na matukio ya maafa kupitia utaratibu uliowekwa, matumizi

ya rasilimali na kuzingatia masuala mtambuka.

Mikakati inayolenga kutambua hatari za maafa kabla hayajatokea imeainishwa kupitia uelewa wa hatari za maafa, na kwa kutambua ni lini yanakaribia kutokea au yanapotokea kupitia utabiri na tahadhari za awali. Hatua za kukabiliana nazo zimeainishwa katika kuzuia, kupunguza madhara na kujiandaa, kukabili na kurejesha hali. Utaratibu na usimamizi wa rasilimali umeainishwa katika usimamizi wa hatari ya maafa na uwekezaji ufadhili katika sekta ya umma na binafsi, na masuala mtambuka yameainishwa kwa kuzingatia jinsia, makundi yaliyo katika mazingira hatarishi na tofauti za kiutamaduni, majukumu ya kikanda na kimataifa na masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Mikakati haifanyi kazi yenyewe, lakini pia inategemea kila mmoja kwa njia ambayo utendaji wa kazi moja unahitaji matokeo kutoka kwa kazi nyingine, kwa mfano: taarifa kwa umma kuhama katika maeneo hatarishi zitategemea utabiri na taarifa za tahadhari ya awali kutoka katika mamlaka husika zinazoonesha uwezekano wa mafuriko kutokea.

# SEHEMU YA TATU

## 3.0 DIRA, DHIMA NA MALENGO

### 3.1 Dira

Kuwa na jamii yenye ufanisi na uwezo wa kuzingatia vihatarishi na kukabiliana na maafa kwa maendeleo endelevu.

### 3.2 Dhima

Kuchukua hatua stahiki na madhubuti za kupunguza na kudhibiti hatari za maafa ili kuokoa maisha, na kulinda mali, mazingira na uchumi kwa ustahimilivu wa taifa.

### 3.3 Malengo

#### 3.3.1 Lengo kuu

Kuimarisha ustahimilivu wa taifa dhidi ya maafa kwa kuchukua hatua jumuishi, kamili na yakinifu katika usimamizi wa maafa.

#### 3.3.2 Malengo mahususi

(a) Kuongeza uelewa wa vihatarishi vya maafa katika ngazi zote.

(b) Kuimarisha uwezo wa kuzuia, kupunguza madhara na kujiandaa na maafa katika ngazi zote kwa ajili ya ustahimilivu wa jamii.

(c) Kuboresha mifumo changamano ya tahadhari ya mapema ya majanga tofauti tofauti kwa kuzingatia mahitaji ya jamii.

(d) Kuimarisha uwezo wa kukabiliana na maafa na utoaji wa huduma za kibinadamu katika ngazi zote.

(e) Kuongeza uwezo wa kurejesha hali, kukarabati na kujenga upya kwa ubora zaidi kwa ajili ya ustahimilivu wa jamii.

(f) Kuongeza upatikanaji wa rasilimali na uwekezaji katika usimamizi wa maafa kwenye sekta ya umma na binafsi.

(g) Kuimarisha mifumo ya utendaji ya usimamizi wa maafa katika ngazi zote.

(h) Kuimarisha mchangamano wa jinsia, vijana, watu wenye ulemavu na mahitaji ya makundi maalum mengineyo pamoja na utofauti wa tamaduni katika usimamizi wa maafa.

(i) Kuimarisha utekelezaji wa maazimio ya kikanda na kimataifa ambayo yameridhiwa.

(j) Kuimarisha mbinu shirikishi za kisekta katika kudhibiti uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa ajili ya kuhimili maafa.

### 3.4 Kanuni ongozi za usimamizi wa maafa

(a) Serikali ina jukumu la msingi la kuzuia na kupunguza hatari za maafa kwa kushirikiana na wadau wasio wa kiserikali pamoja na ushirikiano wa kimataifa, kikanda na baina ya nchi.

(b) Kuzingatia mbinu kamili na yakinifu, changamano na mfumo wa jamii katika usimamizi wa maafa.

(c) Kushughulikia vihatarishi vya msingi vya maafa kupitia uwekezaji wa umma na binafsi unaozingatia hatari ya maafa na kurejesha hali baada ya maafa (ukarabati na ujenzi) kwa maendeleo endelevu.

(d) Kulenga katika mshikamano unaofaa ili kufikia maendeleo endelevu, usalama wa chakula, afya dhabiti, mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi, usimamizi wa mazingira na kupunguza hatari ya maafa.

(e) Usimamizi wa utoaji wa misaada ya kibinadamu kwa njia ya usawa, thabiti na inayokubalika.

(f) Taarifa za usimamizi wa maafa zitatolewa kwa popote inapowezekana ili kuhakikisha ufanyaji maamuzi sahihi.

(g) Ukuaji wa ujuzi na utaalam utaimarishwa kupitia kumbukumbu za utendaji bora, uzoefu na matokeo ya utafiti wa kijamii na kisayansi.

# SEHEMU YA NNE

## 4.0 UTEKELEZAJI WA MKAKATI

### 4.1 Uelewa wa vihatarishi vya maafa

**(a) Lengo**

Kuongeza uelewa wa vihatarishi vya maafa katika ngazi zote

**(b) Mikakati**

(i) Kufanya tathmini za kina za hatari za maafa za mara kwa mara katika ngazi zote, kuanzia pale inapowezekana kutokana na vipaumbele vilivyoainishwa na Profaili ya Maafa.

(ii) Matumizi ya taarifa za tathmini ya hatari ya maafa zinazopatikana kwa wakati husika kwa ajili ya kuandaa mipango ya maendeleo kwa lengo la kukuza matumizi ya taarifa za vihatarishi katika kuweka vipaumbele vya kiutendaji pamoja na maandalizi ya mikakati na sera

(iii) Kujumuisha usimamizi wa maafa katika mifumo na mitaala ya elimu ya juu na ya kiufundi pamoja na ajenda ya utafiti ya taifa.

(iv) Kuhamasisha tafiti za usimamizi wa maafa kwa kushirikiana na wadau.

(v) Kuwezesha uundaji wa majukwaa ya wadau, mitandao na mifumo ya kushirikishana taarifa zinazohusu usimamizi wa maafa.

(vi) Kukuza matumizi ya TEHAMA na taarifa za kijiografia katika usimamizi wa maafa.

(vii) Kutekeleza kampeni ya uhamasishaji wa uelewa wa hatari ya maafa kwa kuzingatia mwenendo wa hatari zinazoweza kutokea pamoja na mahitaji maalum kwa watu wenye ulemavu.

(viii) Kuandaa mkakati wa kushawishi wa masuala ya usimamizi wa maafa na kufanya kampeni za

ushawishi kwa watoa maamuzi kwa kuzingatia mwenendo wa matukio ya hatari za maafa katika sekta.

**(c) Shabaha**

(i) Tathmini ya kina ya hatari ya maafa na ramani za majanga makuu kumi kufanyika katika ngazi zote ifikapo 2027.

(ii) Taarifa za kina za hatari ya maafa kuzingatiwa katika utaratibu wa kuandaa mipango ya kisekta ifikapo 2027.

(iii) Mitaala ya usimamizi wa maafa na nyenzo za mafunzo kuandaliwa na kujumuishwa katika mfumo wa elimu ya juu na ufundi kwa kuzingatia ushahidi wa kisayansi unaotokana na tafiti za tathmini ya hatari ya maafa ifikapo 2027

(iv) Utafiti wa matuko wa pamoja kati ya jamii, taasisi za utafiti na taasisi za elimu zilizohusika na usimamizi wa maafa unafanyika ifikapo 2027.

(v) Jukwaa la utafiti wa usimamizi wa maafa na mtandao kuanzishwa ifikapo 2027.

(vi) Majukwaa na mitandao ya kushirikishana taarifa za usimamizi wa maafa kuanzishwa katika ngazi zote ifikapo 2024.

(vii) Taarifa za uhakika za wakati husika kuhusu usimamizi wa maafa kwa ajili ya wadau wote zinapatikana ifikapo Juni 2025.

(viii) Mikataba husika ya kikanda na kimataifa ya upatikanaji wa huduma za TEHAMA na taarifa za kijiografia inazingatiwa ifikapo 2027.

(ix) Matumizi ya takwimu za picha za anga katika kupunguza hatari ya maafa kuboreshwa ifikapo 2027.

(x) Miongozo ya matumizi ya TEHAMA na huduma za kijiografia katika usimamizi wa maafa kuandaliwa ifikapo 2027.

(xi) Kampeni ya uhamasishaji kuhusu hatari ya maafa kuendeshwa katika ngazi zote ikizingatia uwezekano wa matukio ya maafa ifikapo 2027.

(xii) Mkakati wa ushawishi wa usimamizi wa maafa kuandaliwa na kufanya kampeni ya ushawishi kwa watoa maamuzi kwa kuzingatia mwenendo wa matukio ya hatari za maafa katika sekta kifikapo 2027.

## 4.2 Kuzuia, kupunguza madhara na kujiandaa na maafa

### (a) Lengo

Kuimarisha uwezo wa kuzuia, kupunguza madhara na kujiandaa na maafa katika ngazi zote kwa ajili ya ustahimilivu wa jamii.

### (b) Mikakati

(i) Kuandaa miongozo ya namna ya kuzingatia masuala ya usimamizi wa maafa katika mipango ya maendeleo ya kisekta, mikakati, bajeti na programu katika ngazi zote.

(ii) Kuhamasisha matumizi ya bima katika usimamizi wa maafa.

(iii) Kufanya mafunzo na mazoezi ya vitendo ya mara kwa mara katika ngazi zote.

(iv) Kuimarisha uwezo wa kutumia dhana ya afya moja kwa maafa husika yanayohusiana na masuala ya afya katika ngazi zote kwa ustahimilivu wa jamii.

(v) Kuandaa ramani na kuanzisha vituo vya kujihifadhi katika maeneo hatarishi kwa maafa.

(vi) Kujenga uwezo wa tathmini ya uharibifu na mahitaji katika ngazi zote.

(vii) Kuwezesha kurejea na kuandaa vigezo vya majenzi, kanuni na miongozo ya usalama.

(viii) Kuimarisha huduma za kinga za afya kwa magonjwa ya mlipuko.

(ix) Kuhamasisha mgawanyo na mipango ya usimamizi na matumizi ya ardhi katika miji na vijiji.

(x) Kuhamasisha matumizi ya mbinu bora za usimamizi maafa.

(xi) Kuandaa mikakati ya usimamizi wa maafa na mipango ya kujiandaa kukabiliana na maafa kwa kuzingatia tathmini ya hatari za maafa za kisayansi inapowezekana katika ngazi zote.

(xii) Kuimarisha uwezo wa taasisi zinazotoa huduma za utafutaji na uokoaji kuwa na vifaa vya kisasa.

(xiii) Kuanzisha huduma za matibabu ya dharura katika ngazi ya mkoa.

**(c) Shabaha**

(i) Miongozo ya namna ya kuzingatia masuala ya usimamizi wa maafa katika mipango ya maendeleo ya kisekta, mikakati, bajeti na programu katika ngazi zote kuandaliwa ifikapo 2025.

(ii) Kuzijengea uwezo sekta wa namna ya kuzingatia masuala ya usimamizi wa maafa katika mipango ya maendeleo ifikapo 2027.

(iii) Matumizi ya bima katika usimamizi wa maafa kuhamasishwa ifikapo 2027.

(iv) Mafunzo na mazoezi ya vitendo ya mara kwa mara katika ngazi zote kufanya ifikapo 2027.

(v) Mafunzo, mazoezi ya kawaida na vitendo ya usimamizi wa hatari zinazovuka mipaka kufanyika ifikapo 2027.

(vi) Uwezo wa kutumia dhana ya afya moja kwa maafa husika yanayohusiana na masuala ya afya katika ngazi zote kwa ustahimilivu wa jamii kuimarisha ifikapo 2027.

(vii) Zana na programu za usimamizi wa magonjwa ya milipuko na wadudu wanaohama kuandaliwa, kuwianishwa na kutekelezwa ifikapo 2027.

(viii) Ramani kuandaliwaa na vituo vya kujihifadhi katika maeneo hatarishi kwa maafa kuanzishwa ifikapo 2027.

(ix) Uwezo wa kufanya tathmini ya uharibifu na mahitaji kuimarishwa katika ngazi zote ifikapo 2027.

(x) Kuwezesha vigezo vya majenzi, kanuni na miongozo ya usalama kurejewa na kuandaliwa ifikapo 2027.

(xiv) Huduma za kinga za afya kwa magonjwa ya mlipuko kuimarishwa ifikapo 2027.

(xv) Mgawanyo na mipango ya usimamizi na matumizi ya ardhi katika miji na vijiji kuimarishwa ifikapo 2027.

(xvi) Mbinu bora za usimamizi wa maafa kutambuliwa na kushirikishwa kwa wadau ifikapo 2027.

(xvii) Mikakati ya usimamizi wa maafa na mipango ya kujiandaa kukabiliana na maafa inayozingatia tathmini ya hatari za maafa za kisayansi inapowezekana kuandaliwa katika ngazi zote ifikapo 2027.

(xviii) Uwezo wa taasisi zinazotoa huduma za utafutaji na uokoaji kuwa na vifaa vya kisasa kuimarishwa ifikapo 2027.

(xix) Huduma za matibabu ya dharura katika ngazi ya mkoa kuimarishwa ifikapo 2027.

## 4.3 Mfumo changamano wa tahadhari ya mapema

**(a) Lengo**

Kuboresha mifumo changamano ya tahadhari ya mapema ya majanga tofauti tofauti kwa kuzingatia mahitaji ya jamii.

**(b) Mikakati**

(i) Kuwezesha taasisi zinazo husika na tahadhari ya mapema na operesheni za dharura kuandaa na kuzingatia uwepo wa jukwaa la pamoja la mawasiliano ya sekta mbalimbali.

(ii) Kuimarisha uwezo wa Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura kufanya kazi kikamilifu kwa saa 24 kwa siku 7 za wiki kwa kuwa na vifaa na teknolojia ya kisasa pamoja na watumishi wenye utaalam waliopata mafunzo vyema.

(iii) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA na teknolojia ya taarifa za kijiografia katika utabiri, ufuatiliaji na usambazaji wa taarifa za tahadhari kwa umma na watu walio katika mazingira hatarishi kwa wakati na kwa njia inayotambulika kwa urahisi.

(iv) Kujumuisha maarifa ya wenyeji katika mifumo rasmi ya tahadhari ya mapema.

(v) Kuandaa taratibu za kawaida za uendeshaji na hadidu za utoaji wa taarifa za taadhari ya mapema.

(vi) Kuongeza uelewa kuhusu taarifa za tahadhari ya mapema kwa makundi maalum.

**(c) Shabaha**

(i) Uwezo wa taasisi zinazohusika na taadhari ya mapema na operesheni za dharura kuimarishwa ifikapo 2027.

(ii) Jukwaa la pamoja la kiteknolojia ya habari na

mawasiliano la taarifa za usimamizi wa maafa na mfumo wa ubadilishanaji wa takwimu ili kusaidia taasisi zote zenye kuhusika na taadhari ya mapema kuunganishwa na Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura pamoja na utaratibu wa pamoja wa kutoa tahathari za mapema kwa umma kuanzishwa ifikapo 2027.

(vii) Matumizi ya TEHAMA na teknolojia ya taarifa za kijiografia katika utabiri, ufuatiliaji na usambazaji wa taarifa za tahadhari kwa umma na watu walio katika mazingira hatarishi kwa wakati na kwa njia inayotambulika kwa urahisi kuimarishwa ifikapo 2027.

(iii) Utafiti na urasimishaji wa maarifa ya jadi katika tahathari ya mapema kuwezeshwa ifikapo 2027.

(iv) Taratibu za kawaida za uendeshaji na hadidu za utoaji wa taarifa za taadhari ya mapema kuandaliwa ifikapo 2027.

(v) Ujumbe wa tahadhari ya mapema unaozingatia mahitaji ya mtumiaji wa mwisho ili kutoa mwelekeo wa hatua za kuchukua kwa makundi yaliyolegwa kupitia mifumo ya habari (radio, runinga, mitandao ya kijamii, magazeti, n.k.,) kuandaliwa ifikapo 2027.

## 4.4 Uwezo wa kukabiliana na maafa na huduma za kibinadamu

### (a) Lengo

Kuimarisha uwezo wa kukabiliana na maafa na utoaji wa huduma za kibinadamu katika ngazi zote.

### (b) Mikakati

(i) Kuanzisha na kuimarisha timu za kukabiliana na maafa zinazojumuisha Wataalam kutoka sekta mbalimbali katika ngazi ya Taifa, Mikoa na wilaya.

(ii) Kuandaa na kutekeleza mpango wa dharura wa taifa na kisekta.

(iii) Kuandaa miongozo, taratibu na vigezo vya afua za kukabiliana na maafa za kitaifa.

(iv) Kuandaa miongozo na taratibu za uratibu wa kukabiliana na maafa yanayovuka mipaka.

(v) Kuimarisha uwezo wa kiutendaji pamoja na upatikanaji wa vifaa vya misaada ya kibinadamu katika maghala ya kikanda ili kutoa huduma kwa waathirika kwa wakati.

(vi) Kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara na kutunza orodha ya uwezo wa kukabiliana na maafa katika ngazi zote.

(vii) Kuimarisha huduma ya lishe na usaidizi unaohitajika kwa jamii wakati wa dharura na maafa.

**(a) Shabaha**

(i) Timu za kukabiliana na maafa zinazojumuisha Wataalam kutoka sekta mbalimbali katika ngazi ya Taifa, Mikoa na wilaya kuanzishwa na kuimarishwa ifikapo 2025.

(ii) Mpango wa dharura wa taifa na kisekta kuandaa na kutekelezwa kwa kuzingatia ufahamu wa vihatarishi uliopatikana kutoka katika taarifa za tathmini za vihatarishi ifikapo 2024.

(iii) Mwongozo wa viwango vya msingi kwa ajili ya kutoa huduma za kibinadamu kuandaliwa ifikapo 2024.

(iv) Miongozo na taratibu za uratibu wa kukabiliana na maafa yanayovuka mipaka kuandaliwa na kuwekewa uratibu ifikapo 2027.

(v) Bajeti ya vifaa katika maghala ya kimkakati na mpango wa kuhifadhi kuandaliwa na kutekelezwa ifikapo 2027.

(viii) Ufuatiliaji wa mara kwa mara na kutunza orodha ya uwezo wa kukabiliana na maafa

katika ngazi zote kufanyika ifikapo 2027.

(ix) Huduma ya lishe na usaidizi unaohitajika kwa jamii wakati wa dharura na maafa kuimarishwa ifikapo 2027.

## 4.5 Kurejesha hali, kukarabati na kujenga upya kwa ubora zaidi

### (a) Lengo

Kuongeza uwezo wa kurejesha hali, kukarabati na kujenga upya kwa ubora zaidi kwa ajili ya ustahimilivu wa jamii.

### (b) Mikakati

(i) Kuandaa miongozo na viwango vya kurejesha hali baada ya maafa.

(ii) Mapitio ya hatua za kukabili maafa na kuandaa masuala ya kujifunza kwa ajili ya kujumuishwa katika hatua za baadaye za usimamizi wa maafa.

(iii) Kujumuisha utoaji wa usaidizi wa kisaikolojia na huduma ya afya ya akili na urekebishaji kwa watu wote wanaohitaji wakati wa dharura na wakati wa hatua za kurejesha hali.

(iv) Kuhakikisha utoaji wa huduma za hifadhi ya jamii kwa makundi yaliyopo katika mazingira hatarishi ikiwa ni pamoja na uhamilishaji wa fedha kwa ajili ya kurejesha hali pale inapowezekana.

(v) Kufanya tathmini ya mahitaji baada ya maafa kutokea kwa matukio makubwa ili kuzingatia wakati wa kurejesha hali.

### (c) Shabaha

(i) Miongozo na viwango vya kurejesha hali baada ya maafa (kukarabati na kujenga upya) kuandaliwa ifikapo 2024.

(ii) Miongozo ya kuzingatia hatari ya maafa katika kurejesha hali (kurabati na kujenga upya) katika

sekta ikiwezekana kwa kuzingatia ukokotoaji wa gharama na faida kuandaliwa ifikapo 2024.

(iii) Rasilimali za kufanya tathmini baada ya maafa kutafutwa ifikapo 2027.

(iv) Mipango ya usimamizi wa maafa kurejewa ili kujumjuisha masuala ya kujifunza ifikapo 2027.

(v) Utoaji wa usaidizi wa kisaikolojia na huduma ya afya ya akili na urekebishaji kwa watu wote wanaohitaji kukumuishwa wakati wa dharura na wakati wa hatua za kurejesha hali ifikapo 2027.

(vi) Miongozo ya utoaji wa huduma za hifadhi ya jamii kwa makundi yaliyopo katika mazingira hatarishi ikiwa ni pamoja na uhamilishaji wa fedha pale inapowezekana kwa ajili ya kurejesha hali kuandaliwa ifikapo 2027.

(vii) Tathmini ya mahitaji baada ya maafa makubwa kufanyika ifikapo 2027.

(viii) Mwongozo wa utafutaji wa rasilimali za kurejesha hali kuandaliwa ifikapo 2024.

(ix) Mfumo wa Taifa wa Kurejesha Hali kuandaliwa ifikapo 2023.

### 4.6 Rasilimali na uwekezaji katika usimamizi wa maafa kwenye sekta ya umma na binafsi

**(a) Lengo**

Kuongeza upatikanaji wa rasilimali na uwekezaji katika usimamizi wa maafa kwenye sekta ya umma na binafsi.

**(b) Mikakati**

(i) Kuanzisha mfumo wa taifa wa uwekezaji katika usimamizi wa maafa na mkakati wa utafutaji rasilimali.

(ii) Kuanzisha mfumo wa uendeshaji wa ufadhili wa hatari za maafa, bima na ulinzi wa kifedha katika uwekezaji wa umma na binafsi kulingana na ukokotoaji wa makadirio ya madhara.

(iii) Kuwezesha uimarishaji wa mitandao ya usalama wa kijamii na Voluntia kuleta ufanisi wa usimamizi wa maafa.

(iv) Kubuni hatua za motisha ili kuhamasisha uwekezaji katika usimamizi wa maafa.

**(c) Shabaha**

(i) Mfumo wa taifa wa uwekezaji katika usimamizi wa maafa na mkakati wa utafutaji rasilimali kuandaliwa ifikapo 2024.

(ii) Mfumo wa uendeshaji wa ufadhili wa hatari za maafa, bima na ulinzi wa kifedha katika uwekezaji wa umma na binafsi kulingana na ukokotoaji wa makadirio ya madhara kuanzishwa ifikapo 2027.

(iii) Mitandao ya usalama wa kijamii na Voluntia kuimarishwa kuleta ufanisi wa usimamizi wa maafa ifikapo 2027.

(iv) Hatua za motisha ili kuhamasisha uwekezaji katika usimamizi wa maafa kuanzishwa ifikapo 2024.

## 4.7 Mfumo wa utendaji wa usimamizi wa maafa

**(a) Lengo**

Kuimarisha mifumo ya utendaji ya usimamizi wa maafa katika ngazi zote.

**(b) Mikakati**

(i) Kuimarisha uratibu wa utekelezaji wa sera na sheria kwa kuzingatia mfumo katika ngazi zote.

(ii) Kuhakikisha ujenzi na uwepo wa vifaa katika Kituo cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa.

(iii) Kukuza utamaduni wa kuzingatia taratibu, sheria na kanuni kuhusu usimamizi wa maafa kuanzia shule za msingi hadi taasisi za elimu ya juu.

(iv) Kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu ya usimamizi wa maafa.

(v) Kuandaa mfumo wa kitaifa wa matumizi ya TEHAMA katika usimamizi wa maafa.

**(c) Shabaha**

(i) Kanuni, taratibu na miongozo ya uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa maafa kuandaliwa ifikapo 2027.

(ii) Masuala ya usimamizi wa maafa kujumuisha katika mpango wa kitaifa na mwongozo wa bajeti kwa ajili ya kuzingatiwa katika sekta zote ifikapo 2027.

(iii) Kituo cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa kujengwa na kuwezeshwa kwa vifaa ifikapo 2027.

(iv) Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Maafa ya 2004 kurejewa ifikapo 2024.

(v) Kushawishi kuzingatiwa masuala ya usimamizi wa maafa katika mfumo wa ajira wa serikali ifikapo 2027.

(vi) Utamaduni wa kuzingatia taratibu, sheria na kanuni kuhusu usimamizi wa maafa kuanzia shule za msingi hadi taasisi za elimu ya juu kuimarishwa ifikapo 2027.

(vii) Programu za kujenga uwezo wa mfumo wa usimamizi wa maafa kuandaliwa na kutekelezwa ifikapo 2027.

(viii) Uwezo wa kamati za usimamizi wa maafa kuimarishwa katika ngazi zote ifikapo 2027.

(ix) Utekelezaji wa sheria zinazohusiana na

usimamizi kuimairishwa katika sekta zote ifikapo mwaka 2027.

(x) Kuanzisha ushirika wa sekta binafsi katika masuala ya usimamizi wa maafa kuanzishwa kwa kuzingatia Ushirikiano wa Sekta Binafsi wa Kimataifa uliopo ifikapo 2024

(xi) Mfumo wa kitaifa wa matumizi ya TEHAMA katika usimamizi wa maafa kuandaliwa ifikapo 2024.

## 4.8 Jinsia, vijana, watu wenye ulemavu na mahitaji ya makundi maalum mengineyo pamoja na utofauti wa tamaduni

### (a) Lengo

Kuimarisha mchangamano wa jinsia, vijana, watu wenye ulemavu na mahitaji ya makundi maalum mengineyo pamoja na utofauti wa tamaduni katika usimamizi wa maafa.

### (b) Mikakati

(i) Kuzingatia vipaumbele na ushiriki wa watu wenye ulemavu na makundi maalum mengineyo katika usimamizi wa maafa.

(ii) Kuhakikisha uwepo na utekelezaji wa program maalum zilizoandaliwa kwa ajili ya kujenga uwezo kuhusu usalama na ustahimilivu kwa makundi maalum.

(iii) Kujumuisha mahitaji ya jinsia, vijana, watu wenye ulemavu na makundi maalum mengineyo katika sera ya usimamazini wa maafa, program na miongozo ya uendeshaji.

(iv) Kuzingatia utofauti wa tamaduni katika masuala ya usimamizi wa maafa.

### (c) Shabaha

(i) Mwongozo wa kuzingatia vipaumbele na

ushiriki wa watu wenye ulemavu na makundi maalum mengineyo katika usimamizi wa maafa kuandaliwa ifikapo 2027.

(ii) Programu maalum kwa ajili ya kujenga uwezo kuhusu usalama na ustahimilivu kwa makundi maalum kuandaliwa na kutekelezwa ifikapo 2027.

(iii) Mwongozo wa kuzingatia mahitaji ya jinsia, vijana, watu wenye ulemavu na makundi maalum mengineyo katika sera ya usimamazini wa maafa, program na miongozo ya uendeshaji kuandaliwa ifikapo 2027.

(iv) Mahitaji ya makundi maalum ikiwemo wakimbizi na watu waliohama makazi kujumuishwa katika awamu zote za usimamizi wa maafa ifikapo 2027.

(v) Utofauti wa tamaduni kuzingatiwa katika masuala ya usimamizi wa maafa ifikapo 2027.

## 4.9 Ushirikiano wa kikanda na kimataifa

### (a) Lengo

Kuimarisha utekelezaji wa maazimio ya kikanda na kimataifa ambayo yameridhiwa.

### (b) Mikakati

(i) Kutekeleza makubaliano na mikataba baina ya nchi mbili, kikanda na kimataifa katika nyanja zote za usimamizi wa maafa.

(ii) Kuhakikisha ushiriki katika mikutano ya kikanda na kimataifa, mafunzo, semina na mazoezi ya usimamizi wa maafa.

(iii) Kuhimiza maandalizi ya mifumo ya kitaifa, kikanda na kimataifa ya gharama nafuu na matumizi rahisi pamoja na huduma ya kubadilishana taarifa kuhusu utendaji mzuri katika usimamizi wa maafa na huduma za

kibinadamu.

(iv) Kuhimiza ushirikiano wa kikanda na kimataifa kwa taasisi za tafiti za kitaaluma na kisayansi na mitandao ya usimamizi wa maafa.

(v) Kuweka au kushiriki katika mifumo iliyopo ya ufuatiliaji wa kiwango cha utekelezaji wa makubaliano na mikataba ya pande mbili, kikanda na kimataifa katika nyanja zote za usimamizi wa maafa.

**(c) Shabaha**

(i) Makubaliano na mikataba baina ya nchi mbili, kikanda na kimataifa katika nyanja zote za usimamizi wa maafa kutekelezwa ifikapo 2027.

(ii) Mikataba ya kikanda na kimataifa ya usimamizi wa maafa na mingine muhimu ya kushughulikia maafa yanayovuka mipaka kutekelezwa ifikapo 2027.

(iii) Ushiriki katika mikutano ya kikanda na kimataifa, mafunzo, semina na mazoezi ya usimamizi wa maafa kuhimizwa ifikapo 2027.

(iv) Ushiriki katika mipango ya kukuza ushirikiano kikanda na kimataifa ya usimamizi wa maafa na huduma za kibinadamu kuhimizwa ifikapo 2027.

(v) Mifumo ya kitaifa, kikanda na kimataifa ya gharama nafuu na matumizi rahisi pamoja na huduma ya kubadilishana taarifa kuhusu utendaji mzuri katika usimamizi wa maafa na huduma za kibinadamu kuandaliwa na kutekelezwa ifikapo 2027.

(vi) Ushirikiano wa kikanda na kimataifa kwa taasisi za tafiti za kitaaluma na kisayansi na mitandao ya usimamizi wa maafa kukuzwa ifikapo 2027.

(vii) Mifumo ya ufuatiliaji wa kiwango cha utekelezaji wa makubaliano na mikataba ya pande mbili,

kikanda na kimataifa katika nyanja zote za usimamizi wa maafa kutekelezwa ifikapo 2027.

## 4.10 Hifadhi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi

### (a) Lengo

Kuimarisha mbinu shirikishi za kisekta katika kudhibiti uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa ajili ya kuhimili maafa.

### (b) Mikakati

(i) Kuimarisha ujumuishaji wa masuala ya usimamizi wa maafa katika mabadiliko ya tabianchi, uhifadhi wa mazingira na maendeleo endelevu.

(ii) Kukuza utekelezaji wa pamoja wa hatua za usimamizi wa maafa na mikakati ya mabadiliko ya tabianchi.

(iii) Kuhimiza mchangamano wa usimamizi wa maafa katika tathmini ya athari za mazingira.

(iv) Kufanya ushawishi, uelewa na programu za mfumo wa ekolojia kwa kuzingatia usimamizi wa maafa kwa ustahimilivu wa jamii.

(v) Kukuza teknolojia na uvumbuzi kwa ajili ya kudhibiti mabadiliko ya tabianchi yanayohusiana na hatari za maafa.

(vi) Kukuza maarifa na kubadilishana taarifa kwa ajili ya usimamizi wa hatari za maafa na kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

### (c) Shabaha

(i) Uwezo wa kujumuisha masuala ya usimamizi wa maafa katika mabadiliko ya tabianchi, uhifadhi wa mazingira na maendeleo endelevu kuimarishwa ifikapo 2027.

(ii) Mfumo wa ekolojia na mazingira kuzingatiwa

katika kufanya tathmini ya hatari ya maafa kitaifa ifikapo 2027.

(iii) Mifano mizuri ya uwekezaji katika miundombinu ya buluu na kijani inayochangia katika kuimarisha ustahimilivu wa maafa kuandikwa kwa rejea ifikapo 2027.

(iv) Usimamizi wa maafa na mikakati ya mabadiliko ya tabianchi kutekelezwa kwa pamoja ifikapo 2027.

(v) Uwekezaji wa kulinda na kuimarisha mifumo ya ekolojia kuzingatiwa kwa ajili ya ustahimilivu wa maafa na mabadiliko ya tabianchi ifikapo 2027.

(vi) Mchangamano wa usimamizi wa maafa katika tathmini ya athari za mazingira na mapendekezo kuzingatiwa ifikapo 2027.

(vii) Ushawishi, uelewa na programu za mfumo wa ekolojia kwa kuzingatia usimamizi wa maafa kwa ustahimilivu wa jamii kufanyika ifikapo 2027.

(vii) Teknolojia na uvumbuzi kwa ajili ya kudhibiti mabadiliko ya tabianchi yanayohusiana na hatari za maafa kuimarishwa ifikapo 2027.

(viii) Programu ya kubadilishana uzoefu wa Sera na Mfumo wa pamoja wa usimamizi wa maafa na uhimili wa mabadiliko ya tabianchi kuandaliwa na kutekelezwa ifikapo 2027.

# SEHEMU YA TANO

## 5.0 BANGO KITITA LA UTEKELEZAJI WA MKAKATI

### JEDWALI NA. 2: BANGO KITITA LA MKAKATI

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| (a) Kuongeza uelewa wa vihatarishi vya maafa katika ngazi zote. | (i) Kufanya tathmini za kina za hatari za maafa za mara kwa mara katika ngazi zote, kuanzia pale inapowezekana kutokana na vipaumbele vilivyoainishwa na Profaili ya Maafa. | (i) Tathmini ya kina ya hatari ya maafa na ramani za majanga makuu kumi kufanyika katika ngazi zote ifikapo 2027. | 500,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (ii) Matumizi ya taarifa za tathmini ya hatari ya maafa zinazopatikana kwa wakati husika kwa ajili ya kuandaa mipango ya maendeleo kwa lengo la kukuza matumizi ya taarifa | (ii) Taarifa za kina za hatari ya maafa kuzingatiwa katika utaratibu wa kuandaa mipango ya kisekta ifikapo 2027. | 100,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (iii) za vihatarishi katika kuweka vipaumbele vya kiutendaji pamoja na maandalizi ya mikakati na sera. | | | | |
| | (iv) Kujumuisha usimamizi wa maafa katika mifumo na mitaala ya elimu ya juu na ya kiufundi pamoja na ajenda ya utafiti ya taifa. | (iii) .Mitaala ya usimamizi wa maafa na nyenzo za mafunzo kuandaliwa na kujumuishwa katika mfumo wa elimu ya juu na ufundi kwa kuzingatia ushahidi wa kisayansi unaotokana na tafiti za tathmini ya hatari ya maafa ifikapo 2027. | 200,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (v) Kuhamasisha tafiti za usimamizi wa maafa kwa kushirikiana na wadau. | (iv) Utafiti wa matuko wa pamoja kati ya jamii, taasisi za utafiti na taasisi za elimu zilizohusika na usimamizi wa maafa unafanyika ifikapo 2027.<br><br>(v) Jukwaa la utafiti wa usimamizi wa maafa na mtandao kuanzishwa ifikapo 2027. | 120,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (vi) Kuwezesha uundaji wa majukwaa ya wadau, mitandao na mifumo ya kushirikishana taarifa zinazohusu usimamizi wa maafa. | (vi) Majukwaa na mitandao ya kushirikishana taarifa za usimamizi wa maafa kuanzishwa katika ngazi zote ifikapo 2024. | 50,000,000 | 2024 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (vii) Taarifa za uhakika za wakati husika kuhusu usimamizi wa maafa kwa ajili ya wadau wote zinapatikana ifikapo Juni 2025. | | | • Taasisi za elimu na utafiti |
| | (vii) Kukuza matumizi ya TEHAMA na taarifa za kijiografia katika usimamizi wa maafa. | (viii) Mikataba husika ya kikanda na kimataifa ya upatikanaji wa huduma za TEHAMA na taarifa za kijiografia inazingatiwa ifikapo 2027. | 200,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (ix) Matumizi ya takwimu za picha za anga katika kupunguza hatari ya maafa kuboreshwa ifikapo 2027. | 20,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | | (x) Miongozo ya matumizi ya TEHAMA na huduma za kijiografia katika usimamizi wa maafa kuandaliwa ifikapo 2027. | 50,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (viii) Kutekeleza kampeni ya uhamasishaji wa uelewa wa hatari ya maafa kwa kuzingatia mwenendo wa hatari zinazoweza kutokea pamoja na mahitaji maalum kwa watu wenye ulemavu. | (xi) Kampeni ya uhamasishaji kuhusu hatari ya maafa kuendeshwa katika ngazi zote ikizingatia uwezekano wa matukio ya maafa ifikapo 2027. | 600,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (ix) Kuandaa mkakati wa kushawishi wa masuala ya usimamizi wa maafa na kufanya kampeni za ushawishi kwa watoa maamuzi kwa kuzingatia mwenendo wa matukio ya hatari za maafa katika sekta. | (xii)Mkakati wa ushawishi wa usimamizi wa maafa kuandaliwa na kufanya kampeni ya ushawishi kwa watoa maamuzi kwa kuzingatia mwenendo wa matukio ya hatari za maafa katika sekta kifikapo 2027. | 200,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| (b) Kuimarisha uwezo wa kuzuia, kupunguza madhara na kujiandaa na maafa katika ngazi zote kwa ajili ya ustahimilivu wa jamii. | (i) Kuandaa miongozo ya namna ya kuzingatia masuala ya usimamizi wa maafa katika mipango ya maendeleo ya kisekta, mikakati, bajeti na programu katika ngazi zote. | (i) Miongozo ya namna ya kuzingatia masuala ya usimamizi wa maafa katika mipango ya maendeleo ya kisekta, mikakati, bajeti na programu katika ngazi zote kuandaliwa ifikapo 2025. | 70,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | | (ii) Kuzijengea uwezo sekta wa namna ya kuzingatia masuala ya usimamizi wa maafa katika mipango ya maendeleo ifikapo 2027. | 200,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kuhamasisha matumizi ya bima katika usimamizi wa maafa. | (iii) Matumizi ya bima katika usimamizi wa maafa kuhamasishwa ifikapo 2027. | 100,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (iii) Kufanya mafunzo na mazoezi ya vitendo ya mara kwa mara katika ngazi zote. | (iv) Mafunzo na mazoezi ya vitendo ya mara kwa mara katika ngazi zote kufanya ifikapo 2027.<br>(v) Mafunzo, mazoezi ya kawaida na | 500,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | vitendo ya usimamizi wa hatari zinazovuka mipaka kufanyika ifikapo 2027.<br>(vi) Zana na programu za usimamizi wa magonjwa ya milipuko na wadudu wanaohama kuandaliwa, kuwianishwa na kutekelezwa ifikapo 2027 | | | |
| | (iv) Kuimarisha uwezo wa kutumia dhana ya afya moja kwa maafa husika yanayohusiana na masuala ya afya katika ngazi zote kwa ustahimilivu wa jamii. | (vii) Uwezo wa kutumia dhana ya afya moja kwa maafa husika yanayohusiana na masuala ya afya katika ngazi zote kwa ustahimilivu wa | 700,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (viii) jamii kuimarisha ifikapo 2027. | | | • Taasisi za elimu na utafiti |
| | (v) Kuandaa ramani na kuanzisha vituo vya kujihifadhi katika maeneo hatarishi kwa maafa. | (ix) Ramani kuandaliwaa na vituo vya kujihifadhi katika maeneo hatarishi kwa maafa kuanzishwa ifikapo 2027. | 500,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (vi) Kujenga uwezo wa tathmini ya uharibifu na mahitaji katika ngazi zote. | (x) Uwezo wa kufanya tathmini ya uharibifu na mahitaji kuimarishwa katika ngazi zote ifikapo 2027. | 300,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (vii) Kuwezesha kurejea na kuandaa vigezo vya majenzi, kanuni na miongozo ya usalama. | (xi) Kuwezesha vigezo vya majenzi, kanuni na miongozo ya usalama kurejewa na kuandaliwa ifikapo 2027. | 200,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (viii) Kuimarisha huduma za kinga za afya kwa magonjwa ya mlipuko. | (xii) Huduma za kinga za afya kwa magonjwa ya mlipuko kuimarishwa ifikapo 2027. | 450,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ix) Kuhamasisha mgawanyo na mipango ya usimamizi na matumizi ya ardhi katika miji na vijiji. | (xiii) Mgawanyo na mipango ya usimamizi na matumizi ya ardhi katika miji na vijiji kuimarishwa ifikapo 2027. | 300,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (x) Kuhamasisha matumizi ya mbinu bora za usimamizi maafa. | (xiv) Mbinu bora za usimamizi wa maafa kutambuliwa na kushirikishwa kwa wadau ifikapo 2027. | 150,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (xi) Kuandaa mikakati ya usimamizi wa maafa na mipango ya kujiandaa kukabiliana na maafa kwa kuzingatia tathmini ya hatari za maafa za kisayansi inapowezekana katika ngazi zote. | (xv) Mikakati ya usimamizi wa maafa na mipango ya kujiandaa kukabiliana na maafa inayozingatia tathmini ya hatari za maafa za kisayansi inapowezekana kuandaliwa katika ngazi zote ifikapo 2027. | 750,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (xii) Kuanzisha huduma za matibabu ya dharura katika ngazi ya mkoa | (xvi) Huduma za matibabu ya dharura katika ngazi ya mkoa kuimarishwa ifikapo 2027 | 1,000,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (xiii) Kuimarisha uwezo wa taasisi zinazotoa huduma za utafutaji na uokoaji kuwa na vifaa vya kisasa. | (xvii) Uwezo wa taasisi zinazotoa huduma za utafutaji na uokoaji kuwa na vifaa vya kisasa kuimarishwa ifikapo 2027. | 397,399,483,360 | | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| (c) Kuboresha mifumo changamano ya tahadhari ya mapema ya majanga tofauti tofauti kwa kuzingatia mahitaji ya jamii. | (i) Kuwezesha taasisi zinazo husika na tahadhari ya mapema na operesheni za dharura kuandaa na kuzingatia uwepo wa jukwaa la pamoja la mawasiliano ya sekta mbalimbali. | (i) Uwezo wa taasisi zinazohusika na taadhari ya mapema na operesheni za dharura kuimarishwa ifikapo 2027. | 1,000,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kuimarisha uwezo wa Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura kufanya kazi kikamilifu kwa saa 24 kwa siku 7 za wiki kwa kuwa na vifaa na teknolojia ya kisasa pamoja na watumishi wenye utaalam waliopata mafunzo vyema. | (ii) Jukwaa la pamoja la kiteknolojia ya habari na mawasiliano la taarifa za usimamizi wa maafa na mfumo wa ubadilishanaji wa takwimu ili kusaidia taasisi zote zenye kuhusika na taadhari ya mapema kuunganishwa na Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura pamoja na utaratibu wa pamoja wa kutoa tahathari za mapema kwa umma kuanzishwa ifikapo 2027. | 5,000,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (iii) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA na teknolojia ya taarifa za kijiografia katika utabiri, ufuatiliaji na usambazaji wa taarifa za tahadhari kwa umma na watu walio katika mazingira hatarishi kwa wakati na kwa njia inayotambulika kwa urahisi. | (iii) Matumizi ya TEHAMA na teknolojia ya taarifa za kijiografia katika utabiri, ufuatiliaji na usambazaji wa taarifa za tahadhari kwa umma na watu walio katika mazingira hatarishi kwa wakati na kwa njia inayotambulika kwa urahisi kuimarishwa ifikapo 2027. | 5,000,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (iv) Kujumuisha maarifa ya wenyeji katika mifumo rasmi ya tahadhari ya mapema. | (iv) Utafiti na urasimishaji wa maarifa ya jadi katika tahathari ya mapema kuwezeshwa ifikapo 2027. | 100,000,000 | 2027 | • Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (v) Kuandaa taratibu za kawaida za uendeshaji na hadidu za utoaji wa taarifa za taadhari ya mapema. | (v) Taratibu za kawaida za uendeshaji na hadidu za utoaji wa taarifa za taadhari ya mapema kuandaliwa ifikapo 2027. | 100,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (vi) Kuongeza uelewa kuhusu taarifa za tahadhari ya mapema kwa makundi maalum. | (vi) Ujumbe wa tahadhari ya mapema unaozingatia mahitaji ya mtumiaji wa mwisho ili kutoa mwelekeo wa hatua za kuchukua kwa makundi yaliyolegwa kupitia mifumo | 150,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ya habari (radio, runinga, mitandao ya kijamii, magazeti, n.k.,) kuandaliwa ifikapo 2027. | | | |
| (d) Kuimarisha uwezo wa kukabiliana na maafa na utoaji wa huduma za kibinadamu katika ngazi zote. | (i) Kuanzisha na kuimarisha timu za kukabiliana na maafa zinazojumuisha Wataalam kutoka sekta mbalimbali katika ngazi ya Taifa, Mikoa na wilaya. | (i) Timu za kukabiliana na maafa zinazojumuisha Wataalam kutoka sekta mbalimbali katika ngazi ya Taifa, Mikoa na wilaya kuanzishwa na kuimarishwa ifikapo 2025. | 100,000,000 | 2024 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (ii) Kuandaa na kutekeleza mpango wa dharura wa taifa, mkoa, wilaya na kisekta. | (ii) Mpango wa dharura wa taifa na kisekta kuandaa na kutekelezwa | 500,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (iii) kwa kuzingatia ufahamu wa vihatarishi uliopatikana kutoka katika taarifa za tathmini za vihatarishi ifikapo 2024. | | | • Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (iii) Kuandaa miongozo, taratibu na vigezo vya afua za kukabiliana na maafa za kitaifa. | (iv) Mwongozo wa viwango vya msingi kwa ajili ya kutoa huduma za kibinadamu kuandaliwa ifikapo 2024. | 50,000,000 | 2024 | • MDAs<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (iv) Kuandaa miongozo na taratibu za uratibu wa kukabiliana na maafa yanayovuka mipaka. | (v) Miongozo na taratibu za uratibu wa kukabiliana na maafa yanayovuka mipaka | 150,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (vi) kuandaliwa na kuwekewa uratibu ifikapo 2027. | | | • Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (v) Kuimarisha uwezo wa kiutendaji pamoja na upatikanaji wa vifaa vya misaada ya kibinadamu katika maghala ya kikanda ili kutoa huduma kwa waathirika kwa wakati. | (vii) Bajeti ya vifaa katika maghala ya kimkakati na mpango wa kuhifadhi kuandaliwa na kutekelezwa ifikapo 2027. | 1,000,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (vi) Kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara na kutunza orodha ya uwezo wa kukabiliana na maafa katika ngazi zote. | (viii) Ufuatiliaji wa mara kwa mara na kutunza orodha ya uwezo wa kukabiliana na maafa katika ngazi zote kufanyika ifikapo 2027. | 170,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | • Taasisi za elimu na utafiti |
| | (vii) Kuimarisha huduma ya lishe na usaidizi unaohitajika kwa jamii wakati wa dharura na maafa. | (ix) Huduma ya lishe na usaidizi unaohitajika kwa jamii wakati wa dharura na maafa kuimarishwa ifikapo 2027. | 250,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| (e) Kuongeza uwezo wa kurejesha hali, kukarabati na kujenga upya kwa ubora zaidi kwa ajili ya ustahimilivu wa jamii. | (i) Kuandaa miongozo na viwango vya kurejesha hali baada ya maafa. | (i) Miongozo na viwango vya kurejesha hali baada ya maafa (kukarabati na kujenga upya) kuandaliwa ifikapo 2024. | 50,000,000 | 2024 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (ii) Miongozo ya kuzingatia hatari ya maafa katika kurejesha hali (kurabati na kujenga upya) katika sekta ikiwezekana kwa kuzingatia ukokotoaji wa gharama na faida kuandaliwa ifikapo 2024. | 50,000,000 | 2024 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (ii) Mapitio ya hatua za kukabili maafa na kuandaa masuala ya kujifunza kwa ajili ya kujumuishwa katika hatua za baadaye za usimamizi wa maafa. | (iii) Rasilimali za kufanya tathmini baada ya maafa kutafutwa ifikapo 2027. | 100,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | | (iv) Mipango ya usimamizi wa maafa kurejewa | 100,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (v) ili kujumjuisha masuala ya kujifunza ifikapo 2027. | | | • Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (iii) Kujumuisha utoaji wa usaidizi wa kisaikolojia na huduma ya afya ya akili na urekebishaji kwa watu wote wanaohitaji wakati wa dharura na wakati wa hatua za kurejesha hali. | (vi) Utoaji wa usaidizi wa kisaikolojia na huduma ya afya ya akili na urekebishaji kwa watu wote wanaohitaji kukumuishwa wakati wa dharura na wakati wa hatua za kurejesha hali ifikapo 2027. | 300,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (iv) Kuhakikisha utoaji wa huduma za hifadhi | (vii) Miongozo ya utoaji wa huduma za hifadhi ya jamii | 50,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi |
| | (v) ya jamii kwa makundi yaliyopo katika mazingira hatarishi ikiwa ni pamoja na uhamilishaji wa fedha kwa ajili ya kurejesha hali pale inapowezekana. | (viii) kwa makundi yaliyopo katika mazingira hatarishi ikiwa ni pamoja na uhamilishaji wa fedha pale inapowezekana kwa ajili ya kurejesha hali kuandaliwa ifikapo 2027. | | | • Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (vi) Kufanya tathmini ya mahitaji baada ya maafa kutokea kwa matukio makubwa ili kuzingatia wakati wa kurejesha hali. | (ix) Tathmini ya mahitaji baada ya maafa makubwa kufanyika ifikapo 2027. | 150,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (x)Mwongozo wa utafutaji wa rasilimali za kurejesha hali kuandaliwa ifikapo 2024. | 20,000,000 | 2024 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | | (xi) Mfumo wa Taifa wa Kurejesha Hali kuandaliwa ifikapo 2024. | 50,000,000 | 2024 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| (f) Kuongeza upatikanaji wa rasilimali na uwekezaji katika usimamizi wa maafa kwenye sekta ya umma na binafsi. | (i) Kuanzisha mfumo wa taifa wa uwekezaji katika usimamizi wa maafa na mkakati wa utafutaji rasilimali. | (i) Mfumo wa taifa wa uwekezaji katika usimamizi wa maafa na mkakati wa utafutaji rasilimali kuandaliwa ifikapo 2024. | 50,000,000 | 2024 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (ii) Kuanzisha mfumo wa uendeshaji wa ufadhili wa hatari za maafa, bima na ulinzi wa kifedha katika uwekezaji wa umma na binafsi kulingana na ukokotoaji wa makadirio ya madhara. | (ii) Mfumo wa uendeshaji wa ufadhili wa hatari za maafa, bima na ulinzi wa kifedha katika uwekezaji wa umma na binafsi kulingana na ukokotoaji wa makadirio ya madhara kuanzishwa ifikapo 2027. | 50,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (iii) Kuwezesha uimarishaji wa mitandao ya usalama wa kijamii na Voluntia kuleta ufanisi wa usimamizi wa maafa. | (iii) Mitandao ya usalama wa kijamii na Voluntia kuimarishwa kuleta ufanisi wa usimamizi wa maafa ifikapo 2027. | 50,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (iv) Kubuni hatua za motisha ili kuhamasisha uwekezaji katika usimamizi wa maafa. | (iv) Hatua za motisha ili kuhamasisha uwekezaji katika usimamizi wa maafa kuanzishwa ifikapo 2024. | 50,000,000 | 2024 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| (g) Kuimarisha mifumo ya utendaji ya usimamizi wa maafa katika ngazi zote. | (i) Kuimarisha uratibu wa utekelezaji wa sera na sheria kwa kuzingatia mfumo katika ngazi zote. | (i) Kanuni, taratibu na miongozo ya uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa maafa kuandaliwa ifikapo 2027. | 100,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | | (ii) Masuala ya usimamizi wa maafa kujumuisha katika mpango wa kitaifa na mwongozo wa bajeti kwa ajili ya kuzingatiwa katika sekta zote ifikapo 2027. | 100,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (iii) Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Maafa ya 2004 kurejewa ifikapo 2024. | 300,000,000 | 2024 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | | (iv) Kushawishi kuzingatiwa masuala ya usimamizi wa maafa katika mfumo wa ajira wa serikali ifikapo 2027. | 100,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kukuza utamaduni wa kuzingatia taratibu, sheria na kanuni kuhusu usimamizi wa maafa kuanzia shule za msingi hadi taasisi za elimu ya juu. | (v) Utamaduni wa kuzingatia taratibu, sheria na kanuni kuhusu usimamizi wa maafa kuanzia shule za msingi hadi taasisi za elimu ya juu kuimarishwa ifikapo 2027. | 100,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (iii) Kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu ya usimamizi wa maafa. | (vi) Programu za kujenga uwezo wa mfumo wa usimamizi wa maafa kuandaliwa na kutekelezwa ifikapo 2027. | 300,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (vii) Uwezo wa kamati za usimamizi wa maafa kuimarishwa katika ngazi zote ifikapo 2027. | 800,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | | (viii) Utekelezaji wa sheria zinazohusiana na usimamizi kuimairishwa katika sekta zote ifikapo mwaka 2027. | 75,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (ix) Kuanzisha ushirika wa sekta binafsi katika masuala ya usimamizi wa maafa kuanzishwa kwa kuzingatia Ushirikiano wa Sekta Binafsi wa Kimataifa uliopo ifikapo 2024. | 50,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (iv) Kuandaa mfumo wa kitaifa wa matumizi ya TEHAMA katika usimamizi wa maafa. | (x)Mfumo wa kitaifa wa matumizi ya TEHAMA katika usimamizi wa maafa kuandaliwa ifikapo 2024. | 150,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (v) Kuhakikisha ujenzi na uwepo wa vifaa katika Kituo cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa. | (xi) Kituo cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa kujengwa na kuwezeshwa kwa vifaa ifikapo 2027. | 58,000,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| (h) Kuimarisha mchangamano wa jinsia, vijana, watu wenye ulemavu na mahitaji ya makundi maalum mengineyo pamoja na utofauti wa tamaduni katika usimamizi wa maafa. | (i) Kuzingatia vipaumbele na ushiriki wa watu wenye ulemavu na makundi maalum mengineyo katika usimamizi wa maafa. | (i) Mwongozo wa kuzingatia vipaumbele na ushiriki wa watu wenye ulemavu na makundi maalum mengineyo katika usimamizi wa maafa kuandaliwa ifikapo 2027. | 50,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kuhakikisha uwepo na utekelezaji wa program maalum zilizoandaliwa kwa ajili ya kujenga uwezo kuhusu usalama na ustahimilivu kwa makundi maalum. | (ii) Programu maalum kwa ajili ya kujenga uwezo kuhusu usalama na ustahimilivu kwa makundi maalum kuandaliwa na kutekelezwa ifikapo 2027. | 100,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (iii) Kujumuisha mahitaji ya jinsia, vijana, watu wenye ulemavu na makundi maalum mengineyo katika sera ya usimamazini wa maafa, program na miongozo ya uendeshaji. | (iii) Mwongozo wa kuzingatia mahitaji ya jinsia, vijana, watu wenye ulemavu na makundi maalum mengineyo katika sera ya usimamazini wa maafa, program na miongozo ya uendeshaji kuandaliwa ifikapo 2027. | 50,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (iv) Mahitaji ya makundi maalum ikiwemo wakimbizi na watu waliohama makazi kujumuishwa katika awamu zote za usimamizi wa maafa ifikapo 2027. | 100,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (iv) Kuzingatia utofauti wa tamaduni katika masuala ya usimamizi wa maafa. | (v) Utofauti wa tamaduni kuzingatiwa katika masuala ya usimamizi wa maafa ifikapo 2027. | 50,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| (i) Kuimarisha utekelezaji wa maazimio ya kikanda na kimataifa ambayo yameridhiwa. | (i) Kutekeleza makubaliano na mikataba baina ya nchi mbili, kikanda na kimataifa katika nyanja zote za usimamizi wa maafa. | (i) Makubaliano na mikataba baina ya nchi mbili, kikanda na kimataifa katika nyanja zote za usimamizi wa maafa kutekelezwa ifikapo 2027. | 100,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | | (ii) Mikataba ya kikanda na kimataifa ya usimamizi wa maafa na mingine muhimu ya kushughulikia maafa yanayovuka mipaka kutekelezwa ifikapo 2027. | 200,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kuhakikisha ushiriki katika mikutano ya kikanda na kimataifa, mafunzo, semina na mazoezi ya usimamizi wa maafa. | (iii) Ushiriki katika mikutano ya kikanda na kimataifa, mafunzo, semina na mazoezi ya usimamizi wa maafa kuhimizwa ifikapo 2027. | 100,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | | (iv) Ushiriki katika mipango ya kukuza ushirikiano kikanda na kimataifa ya usimamizi wa maafa na huduma za kibinadamu kuhimizwa ifikapo 2027. | 50,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (iii) Kuhimiza maandalizi ya mifumo ya kitaifa, kikanda na kimataifa ya gharama nafuu na matumizi rahisi pamoja na huduma ya kubadilishana taarifa kuhusu utendaji mzuri katika usimamizi wa maafa na huduma za kibinadamu. | (v) Mifumo ya kitaifa, kikanda na kimataifa ya gharama nafuu na matumizi rahisi pamoja na huduma ya kubadilishana taarifa kuhusu utendaji mzuri katika usimamizi wa maafa na huduma za kibinadamu kuandaliwa na kutekelezwa ifikapo 2027. | 200,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (iv) Kuhimiza ushirikiano wa kikanda na kimataifa kwa taasisi za tafiti za kitaaluma na kisayansi na mitandao ya usimamizi wa maafa. | (vi) Ushirikiano wa kikanda na kimataifa kwa taasisi za tafiti za kitaaluma na kisayansi na mitandao ya usimamizi wa maafa kukuzwa ifikapo 2027. | 50,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (v) Kuweka au kushiriki katika mifumo iliyopo ya ufuatiliaji wa kiwango cha utekelezaji wa makubaliano na mikataba ya pande mbili, kikanda na kimataifa katika nyanja zote za usimamizi wa maafa. | (vii) Mifumo ya ufuatiliaji wa kiwango cha utekelezaji wa makubaliano na mikataba ya pande mbili, kikanda na kimataifa katika nyanja zote za usimamizi wa maafa kutekelezwa ifikapo 2027. | 50,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| (j) Kuimarisha mbinu shirikishi za kisekta katika kudhibiti uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa ajili ya kuhimili maafa. | (i) Kuimarisha ujumuishaji wa masuala ya usimamizi wa maafa katika mabadiliko ya tabianchi, uhifadhi wa mazingira na maendeleo endelevu. | (i) Uwezo wa kujumuisha masuala ya usimamizi wa maafa katika mabadiliko ya tabianchi, uhifadhi wa mazingira na maendeleo endelevu kuimarishwa ifikapo 2027. | 100,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (ii) Mfumo wa ekolojia na mazingira kuzingatiwa katika kufanya tathmini ya hatari ya maafa kitaifa ifikapo 2027. | 50,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | | (iii) Mifano mizuri ya uwekezaji katika miundombinu ya buluu na kijani inayochangia katika kuimarisha ustahimilivu wa maafa kuandikwa kwa rejea ifikapo 2027. | 50,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kukuza utekelezaji wa pamoja wa hatua za usimamizi wa maafa na mikakati ya mabadiliko ya tabianchi. | (iv) Usimamizi wa maafa na mikakati ya mabadiliko ya tabianchi kutekelezwa kwa pamoja ifikapo 2027. | 50,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi, Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | | (v) Uwekezaji wa kulinda na kuimarisha mifumo ya ekolojia kuzingatiwa kwa ajili ya ustahimilivu wa maafa na mabadiliko ya tabianchi ifikapo 2027. | 75,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi,<br>• Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (iii) Kuhimiza mchangamano wa usimamizi wa maafa katika tathmini ya athari za mazingira. | (vi) Mchangamano wa usimamizi wa maafa katika tathmini ya athari za mazingira na mapendekezo kuzingatiwa ifikapo 2027. | 200,000,000 | 2027 | • Wizara, Idara na Taasisi, Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |
| | (iv) Kufanya ushawishi, uelewa na programu za mfumo wa ekolojia kwa kuzingatia usimamizi wa maafa kwa ustahimilivu wa jamii. | (vii) Ushawishi, uelewa na programu za mfumo wa ekolojia kwa kuzingatia usimamizi wa maafa kwa ustahimilivu wa jamii kufanyika ifikapo 2027. | 100,000,000 | 2027 | • Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

| Lengo | Mikakati | Shabaha | Kiasi (TZS) | Muda | Taasisi husika |
|---|---|---|---|---|---|
| | (v) Kukuza teknolojia na uvumbuzi kwa ajili ya kudhibiti mabadiliko ya tabianchi yanayohusiana na hatari za maafa. | (viii) Teknolojia na uvumbuzi kwa ajili ya kudhibiti mabadiliko ya tabianchi yanayohusiana na hatari za maafa kuimarishwa ifikapo 2027. | 200,000,000 | 2027 | • Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa<br>• Wadau wa Maendeleo<br>• Taasisi zisizo za Kiserikali<br>• Taasisi za elimu na utafiti |

# SEHEMU YA SITA

## 6.0 MFUMO WA KISERA, KISHERIA NA KITAASISI

### 6.1 Mfumo wa Kisera

Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya mwaka 2004 inatoa mwongozo wa jumla wa mfumo wa Kisera wa usimamizi wa masuala ya maafa Tanzania Bara. Sera imetambua kuwa maafa ni mtambuka na hivyo kuhitaji ushirikiano wa pamoja baina ya sekta na uwajibikaji wa jamii nzima. Sera inaweka umuhimu katika usalama wa maisha ya watu na mali zao kwa kuhakikisha kupunguza athari za kiuchumi na kijamii ili kujenga uwezo wa uratibu na ushirikiano baina ya wadau muhimu wa maafa katika ngazi zote. Sera imefafanua muundo na majukumu ya usimamizi wa maafa kwa sekta na wadau mbalimbali kuanzia ngazi ya taifa mpaka kijiji. Vile vile, Sera imeeleza majukumu ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Asasi za kiraia, Sekta binafsi, Mashirika ya Umoja wa Mataifa na Kimataifa, Vyombo vya habari na wananchi.

### 6.2 Mfumo wa Kisheria

Mfumo wa Kisheria wa usimamizi wa maafa Tanzania unaongozwa na Sheria ya Usimamizi wa Maafa Sura ya 242. Sheria hiyo imeanzisha mfumo wa Usimamizi wa Maafa kuanzia ngazi ya Taifa hadi Kijiji. Sheria imetoa wajibu kwa sekta na wadau kujumuisha masuala ya maafa katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kuzingatia wajibu wao kisheria.

### 6.3 Mfumo wa Kitaasisi

Ofisi ya Waziri Mkuu ina dhamana ya kuratibu usimamizi wa maafa katika ngazi ya Taifa. Ofisi ina jukumu la kutoa miongozo ya sera, mikakati, mipango, na kanuni kuhusu usimamizi wa maafa. Ofisi ina jukumu la kupanga, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa hatua za kuzuia, kupunguza madhara, kujiandaa, kukabiliana na kurejesha hali kwa kuzingatia hatari zote zinazoweza kutokea. Pia inakuza elimu, maarifa na matumizi ya teknolojia ya mawasiliano ya habari katika usimamizi wa maafa kwa ufahamu wa umma. Kwa mujibu wa Muundo wa Ofisi ya Waziri Mkuu, majukumu ya uratibu na

usimamizi wa maafa yanatekelezwa na Idara ya Menejimenti ya Maafa. Majukumu hayo ni kama ifiuatavyo:-

(i) Kuandaa Sera, Sheria, Mipango na Mikakati ya uratibu na usimamizi wa maafa kwa kushirikiana na wadau;


(ii) Kuratibu masuala ya menejimenti ya maafa nchini kwa kushirikisha sekta mtambuka;

(iii) Kufanya tathmini na tafiti za maafa kwa kushirikiana na sekta, taasisi na wadau mbalimbali; na

(iv) Kuratibu taarifa za tahadhari, kukuza elimu, maarifa, uvumbuzi na matumizi ya teknolojia ya mawasiliano na habari katika usimamizi wa maafa na dhana ya afya moja.

Aidha, ili kuimarisha shughuli za usimamizi wa maafa nchini, Serikali kupitia Sheria ya Usimamizi wa Maafa Sura ya 242 imeweka Mfumo wa Usimamizi wa Maafa ambao umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni upande wa maamuzi na utendaji. Upande wa maamuzi kuna Kamati Elekezi za Usimamizi wa Maafa katika ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya. Upande wa utendaji ni kupitia Kamati za Kitaalam za Usimaimzi wa Maafa za Taifa, Mkoa na Wilaya. Upande utendaji una jukumu la kuchambua na kupendekeza hatua za kitaalam kwa watoa maamuzi ili waweze kutekeleza majukumu yao. Kamati za kitaalam zinaweza kuunda kamati ndogo mbalimbali za wataalam kama vile kikosi maalum au vikundi vya kazi vya kiufundi katika kurahisiaha utekelezaji wa majukumu yake. Katika ngazi Kata na Kijiji/Mtaa kuna Kamati za Usimamizi wa Maafa ambazo hutekeleza majukumu ya usimamizi wa maafa kwenye maeneo yao. Utekelezaji wa shughuli za Kamati umezingatia umuhimu wa kukabidhi majukumu kwa Kamati ya juu iwapo kutatokea kuzidiwa na madhara ya maafa kulingana na rasilimali zilizopo au kuhusishwa kwa Kamati mbili au zaidi zilizopo katika ngazi moja. Muhtasari wa Mfumo wa kitaasisi wa menejimenti ya maafa nchini ni kama unavyoonekana katika Kielelezo Na. 7.

## KIELELEZO NA. 7: MFUMO WA USIMAMIZI WA MAAFA TANZANIA




Chanzo: Ofisi ya Waziri Mkuu

**(a) Kamati Elekezi ya Kitaifa ya Usimamizi wa Maafa**

Kamati Elekezi ya Kitaifa ya Usimamizi wa Maafa inawajibika kutoa maamuzi muhimu, kuweka vipaumbele na kugawa majukumu kabla, wakati na baada ya maafa katika ngazi ya kitaifa. Kamati hii inaongozwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati ina jukumu la kusimamia, kutoa maelekezo na kuweka vipaumbele vya shughuli za usimamizi wa maafa na huduma za kibinadamu katika ngazi ya taifa ikiwa ni pamoja na kuidhinisha Mpango wa Usimamizi wa Maafa na Mpango wa Mwendelezo wa Huduma wakati wa Dharura za Kitaifa

**(b) Kamati ya Wataalam ya Kitaifa ya Usimamizi wa Maafa**

Kamati ya Wataalam ya Kitaifa ya Usimamizi wa Maafa Tanzania inafanya kazi kama chombo cha kitaalamu kwa Kamati ya Elekezi kupendekeza hatua za kuchukua katika

masuala yote yanayohusiana na usimamizi wa maafa yanayotokea katika sekta na wakala nchini. Kamati ina jukumu la kuishauri Kamati Elekezi ya Kitaifa ya Usimamizi wa Maafa hatua za kuimarisha usimamizi wa maafa nchini na kutekeleza maelekezo ya Kamati Elekezi ya Kitaifa ya Usimamizi wa Maafa.

**(c) Jukwaa la Taifa la Wadau wa Usimamizi wa Maafa**

Jukwaa limeanzishwa kwa lengo la kukutanisha wadau mbalimbali kutoka serikalini na nje ya Serikali ili kujadili namna bora ya kuimarisha usimamizi wa maafa kwa ushiriki wa pamoja. Jukwaa ni chombo muhimu kwa ajili ya kuibua changamoto na kujadili namna bora zinavyoweza kutatuliwa kwa kuwa na mikakati shirikishi na upatikanaji wa rasilimali wa haraka pamoja na ufanisi wa utendaji kwa kupunguza muingiliano wa majukumu. Kazi ya jukwaa ni kujadili masuala yanayohusu usimamizi wa maafa na kuishauri Kamati ya Taifa ya Wataalam ya Usimamizi wa Maafa.

**(d) Kamati Elekezi za Mikoa za Usimamizi wa Maafa**

Kamati Elekezi ya Mkoa ya Usimamizi wa Maafa itakuwa na mamlaka ya kutoa maamuzi na maelekezo ya hatua za kuchukua katika usimamizi wa maafa katika ngazi ya Mkoa. Kamati itakua na jukumu la kupanga, kuratibu na kutoa maelekezo kuhusu kushughulikia masuala ya maafa katika Mkoa na kusimamia majukumu ya Kamati ya Wataalam ya Usimamizi wa Maafa ya Mkoa. Mwenyekiti wa kamati Elekezi ya Mkoa ya Usimamizi wa Maafa atakuwa msemaji wa Serikali wakati wa matukio ya maafa katika ngazi ya Mkoa.

**(e) Kamati ya Wataalam ya Mkoa ya Usimamizi wa Maafa**

Kamati ya Wataalam ya Mkoa ya Usimamizi wa Maafa itakuwa na jukumu la kuishauri Kamati Elekezi ya Mkoa kuhusu masuala ya usimamizi wa maafa na mambo mengine yoyote yatakayoelekezwa na Mkuu wa Mkoa. Kamati itawajibika kufuatilia na kuratibu shughuli za upunguzaji na usimamizi wa maafa na huduma za dharura miongoni mwa taasisi za kisekta za Serikali, serikali za mitaa, jamii na wadau wengine wanaojihusisha na maafa.

**(f) Kamati Elekezi ya Wilaya ya Usimamizi wa Maafa**

Kamati Elekezi ya Wilaya ya Usimamizi wa Maafa itakuwa na mamlaka ya kutoa maamuzi na maelekezo ya hatua za kuimarisha na kushughulikia masuala ya maafa katika Wilaya. Kamati itawajibika kupanga, kuratibu na kutoa maelekezo kuhusu kushughulikia masuala ya maafa katika Wilaya husika na kusimamia majukumu ya Kamati ya Wataalam ya Wilaya ya Usimamizi wa Maafa

**(g) Kamati ya Wataalam ya Jiji, Manispaa, Mji na Wilaya ya Usimamizi wa Maafa**

Kamati ya Wataalam ya Jiji, Manispaa, Mji na Wilaya ya Usimamizi wa Maafa itawajibika kutekeleza na kuratibu shughuli za usimamizi wa maafa na uendeshaji wa operesheni za dharura katika ngazi ya Wilaya. Kamati itapendekeza hatua za kitaalam kuhusu masuala yote yanayohusiana na usimamizi wa maafa, kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji washughuli za usimamizi wa maafa na huduma zadharura katika eneo husika kama itakavyoelekezwana Kamati Elekezi ya Wilaya ya Usimamizi waMaafa.

**(h) Kamati ya Kata ya Usimamizi wa Maafa**

Kamati ya Kata ya Usimamizi wa Maafa itakuwa na jukumu la kuhakikisha ushiriki wa wadau wote katika hatua za kuzuia au kupunguza madhara ya majanga pamoja na kutoa huduma za kibinadamu wakati wa dharura. Kamati itawajibika kufuatilia na kuratibu usimamizi wa maafa na operesheni za dharura katika ngazi ya Kata ikiwa ni pamoja na kutafuta rasilimali za usimamizi wa maafa ikiwa ni pamoja na kutafuta rasilimali kwa ajili ya usimamizi wa maafa.

**(i) Kamati ya Kijiji au Mtaa ya Usimamizi wa Maafa**

Kamati ya Kijiji ya Usimamizi wa Maafa itakuwa na wajibu wa awali wa kuhakikisha jamii inakuwa salama dhidi ya majanga pamoja na kushirikisha jamii katika kupata ufumbuzi wa haraka wa huduma za kibinadamu kwa waathirika wa maafa. Kamati itakuwa na jukumu la kufuatilia na kuratibu shughuli za usimamizi wa maafa na operesheni za dharura katika ngazi ya Kijiji au Mtaa ikiwa ni pamoja na kutafuta rasilimali kwa ajili ya usimamizi wa maafa.

### 6.4 Majukumu na wajibu wa watendaji mbalimbali

**(a) Wizara, Idara na Wakala**

Wizara, Idara na Wakala zinapaswa kuwa na kitengo au afisa wa dawati aliyeteuliwa mahsusi kwa ajili ya masuala ya usimamizi wa maafa yanayohusiana na Mkakati wa Taifa wa Uratibu na Usimamizi wa Maafa. Vitengo vitakuwa na jukumu la kuratibu shughuli za usimamizi wa maafa katika sekta/idara/wakala husika. Majukumu ya kisekta katika usimamizi wa maafa ni pamoja na utambuzi wa majanga , tathmini ya hatari na ufuatiliaji, kutoa ushauri juu ya hatua za kupunguza madhara na kuzuia maafa kupitia mipango na bajeti na kujiandaa kwa ajili ya kukabiliana na kurejesha hali. Vikundi kazi vya wataaalam vya usimamizi wa maafa katika kila Sekta vitakua na jukumu la kutoa utaalamu katika hatua za usimamizi wa maafa kwa sekta husika, kuandaa mipango ya usimamizi wa maafa na mipango ya dhrura na Taratibu za Utendaji za Kawaida zinazohusiana na maafa ya kisekta na kuunganisha masuala ya usimamizi wa maafa katika mipango ya maendeleo ya sekta.

**(b) Timu za Kukabiliana na Maafa**

Timu za kukabiliana na maaffa na watu wa kujitolea walioanzishwa katika ngazi zote wanawajibika kukabiliana na maafa na dharura. Taarifa zao ni muhimu kwa ajili ya taarifa za tathmini ambazo zinaweza kutumika kubuni hatua za kuzuia na kupunguza na mipango madhubuti ya kujiandaa na kukabiana na maafa katika katika siku zijazo.

**(c) Sekta Binafsi**

Sekta Binafsi zina utaalamu, vifaa na fedha kwa ajili ya kuiongeza nguvu Serikali katika usimamizi wa maafa. Sekta ina jukumu la kulinda biashara zao kupitia hatua mbalimbali zikiwemo za kuzuia na kupunguza maafa; na uhamisho kama ilivyoonyeshwa katika Mkakati wa Taifa wa Uratibu na Usimamizi wa maafa. Uwekezaji wote unaofanywa unapaswa kuzingatia tathmini ya hatari ya maafa kwa ujumuishaji bora wa kupunguza hatari za maafa kwa uendelevu katika sekta zote.

**(d) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lina jukumu kuu la ukaguzi, kuzuia, kupunguza, ulinzi, utayari na kukabiliana katika operesheni za kuzima moto na uokoaji katika matukio ya moto na majanga mengine. Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji kina ujuzi wa kiufundi kuhusu majanga ya moto na masuala mengine ya dharura yanayohusiana na utafutaji na uokoaji. Watahakikisha matumizi bora vifaa mijini na vijijini. Jeshi litatakiwa kuoanisha utaratibu wa ushiriki wao katika hatua zote za kuzuia na kupunguza katika upangaji na uendeshaji wa sekta ya umma na binafsi katika utekelezaji wa mkakati huu.

**(e) Jeshi la Polisi Tanzania**

Jeshi la Polisi lina majukumu mahususi katika kupunguza, kujiandaa na kukabiliana na maafa katika maeneo ya usalama, uokoaji, usimamizi wa mikusanyiko, msaada wa matibabu ya dharura, mawasiliano na huduma za ofisi. Watalazimika kufanya tathmini ya hatari ya maafa husika kwa ajili ya kupanga, mafunzo na mazoezi ili kuendana na mbinu mpya.

**(f) Taasisi ya Msalaba Mwekundu Tanzania na Chama cha Skauti Tanzania**

Taasisi hizi zimepewa jukumu la kutekeleza majukumu mahususi ya hiari ya kibinadamu katika maafa na dharura kama msaidizi kwa mamlaka ya umma. Wana mitandao ya kimataifa na kitaifa, ambayo ni chanzo muhimu cha wafanyakazi wenye ujuzi na ufadhili. Watashiriki katika uhamasishaji wa jamii kuwa mstari wa kwanza katika kuzuia, kupunguza, kujiandaa na kukabiliana na maafa na utekelezaji wa mkakati huu.

**(g) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania**

Pamoja na majukumu mengine, TCRA inasimamia maendeleo ya miundombinu na huduma za mawasiliano nchini Tanzania ambayo inazingatia masuala kama vile tathmini ya hatari za maafa na Taasisi za tahadhari ya mapema (EWS) kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii. TCRA itahakikisha matumizi ya teknolojia ya habari

na mawasiliano katika kuzuia, kupunguza, kukabiliana na maafa. Zaidi ya hayo, itahakikisha TEHAMA inatumika kama njia ya kusambaza na kubadilishana taarifa miongoni mwa watumiaji mbalimbali kama vile taasisi za umma na binafsi, wataalamu na umma kwa ujumla juu ya hatari inayokaribia ya maafa.

**(h) Asasi za kiraia**

Asasi za Kiraia zina uwezo wa kukusanya rasilimali za ziada, ambazo ni muhimu katika kuongeza juhudi za serikali katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uratibu na Usimamizi wa maafa. Wana faida ya kuwa na ufanisi katika ngazi ya jamii. Kwa hiyo, watakuwa na jukumu la kutatambua majanga, kufanya tathmini ya hatari ya maafa, na kuandaa mapendekezo na mipango ya utekelezaji wa hatua za kijamii za kukabiliana na maafa kwa ajili ya ustahimilivu. Hizi zinaweza kuhusisha programu za uwezeshaji kiuchumi, kujenga uwezo wa kustahimili riziki, kukuza uelewa wa umma, mafunzo, kutoa msaada na kufadhili shughuli za kujisaidia.

**(i) Mashirika ya Kimataifa na Washirika wa Maendeleo**

Umoja wa Mataifa, Mashirika ya Kikanda na Kimataifa ni wadau muhimu katika utekelezaji wa Mkakati wa taifa wa Uratibu na Usimamizi wa maafa kwa sababu yanasaidia juhudi za serikali kwa kutoa misaada ya kifedha, nyenzo na kiufundi. Ushirikiano unapaswa kuimarishwa ili kuimarisha ushirikiano kwa rasilimali zaidi na mahitaji ya utaalamu kwa ajili ya kupunguza hatari ya maafa na utoaji wa huduma za kibinadamu.

**(j) Vyombo vya Habari**

Vyombo vya habari vina jukumu la kipekee na muhimu katika kupunguza na usimamizi wa maafa. Ushirikishanaji wa taarifa baina ya wadau wote ni muhimu katika kuzuia, kupunguza, kujiandaa na kukabiliana na maafa. Vyombo vya habari vinapaswa kuongeza ufahamu wa umma kwa ajili ya tahadhari na uhamasishaji wa rasilimali ili kusaidia kupunguza hatari ya maafa na wakati wa hali ya dharura. Idara zote na taasisi za mafunzo ya vyombo vya habari

zinapaswa kujumuisha masuala ya maafa katika mitaala na shughuli zao za kawaida. Vyombo vya habari vinapaswa kuwajibika zaidi katika kutoa taarifa ya matukio ya maafa kwani taarifa za maafa ni nyeti na zinahitaji uangalizi wa ziada nje ya wajibu wa kawaida katika utoaji.

**(k) Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali**

Pamoja na majukumu mengineWakala umepewa jukumu uchambuzi wa kimaabara wa aina mbalimbali za sampuli ambazo ni muhimu katika hatua mbalimbali za kupunguza hatari za maafa. Sampuli hizi ni pamoja na sampuli zinazohusiana na utambuzi wa wahanga wa maafa, ubora wa bidhaa kwa matumizi mbalimbali ya kijamii na kiuchumi, masuala ya kijamii kama vile utambuzi wa mabaki ya binadamu yaliyosambaratika kutokana na majanga kama vile ajali za moto, baharini, anga na magari, kuporomoka kwa majengo, mlipuko wa bomu na kuzama majini, na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira na afya ya binadamu (wafanyakazi) kama vile sampuli za taka.

**(l) Jumuiya ya Karibu na Familia za Mtu Binafsi**

Jamii na watu binafsi wana jukumu la kutumia uwezo wao wenyewe kulinda maisha na mali zao dhidi ya majanga. Hatua zao ni sehemu muhimu katika mipango ya kupunguza hatari ya maafa kwa utekelezaji wa mkakati huu. Inapaswa kuwa wazi kuwa wao ndio wa kwanza kutambua, kukabiliana na hatari ya maafa na kuwa na jukumu kubwa wakati wa makabiliano ya awali. Vikundi vya jamii kwa ajili ya kupunguza madhara ya maafa na kulinda maisha, tahadhari ya mapema, mawasiliano, huduma ya kwanza na mtandao wa kijamii ni muhimu katika jamii zote.

**(m) Wizara yenye dhamana ya fedha na mipango na taasisi za fedha**

Wizara yenye dhamana ya fedha na mipango na taasisi za fedha itawajibika kuhakikisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya usimamizi wa maafa; kusimamia ujumuishaji wa shughuli za kupunguza hatari za maafa katika sera, mipango, programu na miradi ya maendeleo ya taifa; kuhamasisha rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa programu mbalimbali

za kupunguza hatari za maafa; kuwezesha na kukuza utoaji wa huduma ndogo za fedha yaani mikopo na akiba ili kusaidia programu za kupunguza hatari za maafa. Aidha, Wizara itakuwa na jukumu la kuwezesha uanzishaji upya wa shughuli za kiuchumi (biashara na viwanda) baada ya maafa.

**(n) Wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Majukumu ya wizara yatakuwa ni kuwahamisha na kuwapa makazi watu wanaoishi katika maeneo yenye maafa (k.m. mafuriko, maporomoko ya ardhi); Kufanya tathmini ya maafa kwa majanga jumuishi na kuchora ramani ya hatari; Kuandaa mipango jumuishi ya Wilaya ya Usimamizi wa Maafa; Kuandaa na kutekeleza kampeni za uelimishaji umma kuhusu hatari mbalimbali za maafa; Kuingiza masuala ya Kupunguza Maafa katika mipango ya maendeleo ya wilaya; Kuandaa utaratibu wa utekelezaji wa miongozo na kanuni za ujenzi; Kuandaa na kutekeleza sheria ndogondogo zinazoshughulikia hatua za usimamizi wa maafa; Kuhimiza kilimo-misitu na kukuza upandaji wa miti; Kuandaa na kutekeleza sheria ndogo za kupanga makazi.

## 6.5 Mipango ya kifedha

Usimamizi wa Maafa nchini Tanzania kwa kiasi kikubwa unategemea upatikanaji wa rasilimali kutoka vyanzo vya kimataifa na vya ndani. Njia za ufadhili wa kimataifa ni pamoja na fedha za kimataifa na kikanda pamoja na taasisi za ushirikiano za nchi mbalimbali na washirika wa maendeleo na taasisi binafsi. Mafunzo na kujenga uwezo juu ya utekelezaji wa miradi yatasisitizwa kuimarisha upatikanaji wa vyanzo na fursa mbalimbali za ufadhili.

Ufadhili wa ndani unaweza kupatikana kutoka katika bajeti ya serikali, sekta binafsi, AZAKI pamoja na michango ya mtu binafsi kupitia taratibu mbalimbali katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Sekta ya fedha kama vile benki na mifuko ya hifadhi ya jamii inahimizwa kuchukua nafasi muhimu katika kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mkakati huu. Kwa kuzingatia hili, mbinu jumuishi na mfumo wa kufanya kazi ulioratibiwa unahitajika sana ili kuhakikisha kuwa fedha za kushughulikia usimamizi wa maafa zinakusanywa,

kutengwa na kufuatiliwa ili kufikia malengo yaliyoainishwa katika Mkakati huu.

Usawa wa ufadhili katika mzingo wa usimamizi wa maafa utasisitizwa kulingana na malengo ya mkakati na kuzingatia makubaliano ya kimataifa na kikanda. Usawa huo pia ni muhimu katika kufadhili maeneo mengine kama vile kujenga uwezo, utafiti na maendeleo, ukuzaji na uhamishaji wa teknolojia pamoja na kujenga uelewa.

Kwa ujumla, inatazamiwa kuwa, jumuiya za kimataifa zitaheshimu ahadi na wajibu wao wa katika usimamizi wa maafa kitaifa, kikanda na kimataifa kwa kutoa msaada unaohitajika. Msaada wa kifedha unaotarajiwa kutoka kwa vyanzo vya kigeni, kwa kiasi kikubwa unatarajiwa kuwa katika utaratibu wa ruzuku. Misaada hiyo itazingatia Sheria ya Mikopo na Dhamana, SURA 134 na Sheria ya VAT ya mwaka 2014.

## 7.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI

### 7.1 Utangulizi

Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini umeundwa ili kufuatilia maendeleo na kutathmini utekelezaji wa Mkakati wa Usimamizi wa Maafa. Jukumu la jumla la ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mkakati ni la Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ushirikiano wa karibu na wadau wengine. Kila mdau ataanzisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utakaounganishwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na mifumo mingine ya kitaifa ya ufuatiliaji na tathmini chini ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mpango Elekezi wa Muda Mrefu 2011/12 – 2025/26. Lengo ni kuhakikisha kuwa mifumo ya ufuatiliaji na tathmini katika ngazi mbalimbali inashirikiana kila mmoja. Msisitizo utakuwa katika kuzalisha, kutumia na kujumuisha takwimu husika ili kukidhi mahitaji ya wadau mbalimbali. Ufuatiliaji utafanywa kupitia mikutano, taarifa mahususi na za jumla, usimamizi na ukaguzi

**Madhumuni ya mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ni:** -

(a) Kufuatilia maendeleo wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa katika viwango vya rasilimali na matokeo, kwa kutumia viashiria vya namba na nadharia. Hatua hii inajumuisha mapitio ya mara kwa mara ya ndani ya wizara zote, mikoa, wilaya na kata/vijiji.

(b) Kufuatilia ufanisi na utendaji wa hatua zilizochukuliwa na kutoa maoni ambayo yatawezesha kuboreshwa kwa usimamizi na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa.

(c) Kutoa picha ya kina na inayoboreshwa mara kwa mara ya hali ya utekelezaji wa Mkakati wa Usimamizi wa Maafa kwa umma.

(d) Kuelewa vyema mfumo wa uratibu na utekelezaji na kutoa mwelekeo ili kuweka malengo ya mkakati wa siku zijazo, maelekezo na mikakati.

(e) Kutoa taarifa za tahadhari za awali kuhusu maendeleo yanayohitajika kwa ajili ya mabadiliko /au mapitio ya baadaye; na

(f) Kutoa taarifa kwa wadau wote ambao wana takwimu na taarifa za kutosha zinazohitajika katika ngazi mbalimbali na taasisi mbalimbali za Serikali na Watendaji Wasio wa Serikali.

## 7.2 Malengo ya mfumo wa ufuatiliaji na tathmini

Madhumuni ya jumla ya Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ni kuongoza utekelezaji wa Mkakati. Malengo mahususi ya mfumo ni:-

(a) Kuweka vigezo na viashiria vya ufuatiliaji na tathmini ya mkakati;

(b) Kuweka viashiria vya matokeo ya utekelezaji wa mkakati na kupima matokeo yanayotarajiwa;

(c) Kuongoza watendaji katika shughuli za utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini; na

(d) Kudhibiti matumizi ya rasilimali wakati wa utekelezaji na kutambua fursa za kuboresha.

Mikakati mahususi ya Mfumo wa Ufuatiliaji inajumuisha mbinu shirikishi za aina tofauti tofauti kwa kuzingatia mpangilio maalum ya kitaasisi. Inalenga ukusanyaji wa takwimu, uchambuzi, uhifadhi, usambazaji, mawasiliano, na uhusiano wa kimkakati na mifumo mingine ya ufuatiliaji.

## 7.3 Mpangilio wa kitaasisi wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini

Mpangilio wa kitaasisi ya ufuatiliaji na tathmini ya mkakati utajumuisha mifumo iliyopo kwenye Wizara na Taasisi za umma, hadi ngazi zote zinazohusika na usimamizi wa maafa. Zaidi ya hayo, kutakuwa na viashiria maalum ambavyo vitajumuishwa kupitia Mfumo wa Ufuatiliaji wa Sendai. Hili ni muhimu kwa sababu umuhimu wa viashiria unaweza kutofautiana kulingana na viwango na maeneo kwa ajili ya kuzalisha takwimu na taarifa sahihi na muhimu.

Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa ndani na nje utafanyika ili kurejea utekelezaji wa mkakati. Mfumo wa nje utajumuisha taarifa zinazowasilshwa katika Kamati za Kudumu za Bunge na taasisi zingine za uangalizi. Mfumo wa ndani wa Ufuatiliaji na Tathmini unajumuisha utendaji kazi uliopo katika Wizara, Idara na Taasisi. Hizi zitatathmini kwa utaratibu na kwa umuhimu na kuzingatia malengoa utekelezaji wa mkakati. Vikosi kazi vinavyojumuisha wadau tofauti tofauti vitaanzishwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kuandaa na kutekeleza tathmini na ufuatiliaji pamoja na kutoa mawazo ya

kitaalam na mwelekeo.

### 7.4 Viashiria vya ufuatiliaji na tathmini

Orodha ya viashiria vya nambari na maelezo vimeandaliwa ili kufuatilia maendeleo ya kufikia malengo ya mkakati. Viashiria hivi vitarejewa kila mwaka ili kukidhi mahitaji ya maelezo ya ziada yanayohitajika kwa ajili ya maendeleo mapya. Takwimu za msingi zitakusanywa na kuboreshwa kama kigezo cha msingi cha ufuatiliaji wa utekelezaji wa mkakati.

Katika kila kipindi mahususi cha utekelezaji, tathmini ya ndani na nje itafanywa ili kukagua utekelezaji wa mkakati. Mfumo wa tathmini ya ndani utatathmini kwa utaratibu na kwa malengo utekelezaji wa mkakati. Madhumuni ya jumla ya tathmini ni kuonesha umuhimu, ufanisi na matokeo ya mkakati katika mazingira halisi, maendeleo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi ya nchi.

### 7.5 Zana na matokeo ya ufuatiliaji na tathmini

Zana na matokeo ya mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa Mkakati yatakuwa kama ifuatavyo:

(a) Taarifa za maendeleo kwa kutumia matokeo ya mfumo wa ufuatiliaji, hivyo kufanya mkakati kuwa nyaraka ya kufanyia kazi;

(b) Taarifa za uchanganuzi za tafiti mbalimbali zitakazofanyika; na

(c) Taarifa za utekelezaji wa Mkataba wa Huduma kwa Mteja.

Haya yataonyesha maendeleo katika utekelezaji wa malengo ya mkakati na shabaha zake

## 7.6 Taarifa za ufuatiliaji na tathmini

Jedwali Na. 3: Aina ya taarifa za ufuatiliaji na tathmini

| Aina za taarifa | Yaliyomo | Muda |
|---|---|---|
| I. Taarifa za maendeleo ya mradi na programu | Taarifa Jumuishi inayohusisha shughuli zote zilizofanywa katika mradi | Kila robo na kila mwaka |
| II. Taarifa ya kina ya maendeleo ya usimamizi wa Maafa | Taarifa Jumuishi inayohusu shughuli zote zinazofanywa na taasisi katika masuala ya rasilimali fedha na vifaa. | Kila robo na kila mwaka |
| III. Taarifa ya tathmini | Taarifa za tathmini ya ndani na nje ya programu mbalimbali za utekelezaji | Kila mwaka, Miaka Mitatu na Mitano; |
| IV. Mapitio ya Mkakati | Mapitio ya Mkakati wa Usimamizi wa Maafa. | Baada ya miaka mitano. |

Ofisi ya Waziri Mkuu itatayarisha taarifa kama ifuatavyo:

(a) Taarifa za Tathmini ya Wizara, Idara na Wakala, Mikoa, Halmashauri na taasisi zinazojitegemea;

(b) Taarifa za kila wiki za Idara;

(c) Taarifa za mwezi za Menejimenti ya Ofisi ya Waziri Mkuu;

(d) Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya robo mwaka, nusu ya mwaka na mwaka;

(e) Taarifa za mwaka za Washirika wa Maendeleo; na

(f) Taarifa ya mapitio ya maoni.

## JEDWALI NA. 4: VIASHIRIA VYA UTENDAJI VYA MFUMO WA UFUATILIAJI NA TATHMINI YA USIMAMIZI WA MAAFA

| Malengo ya Kimkakati | Viashiria vya Matokeo | Matarajio/ Athari |
|---|---|---|
| I. Kuongeza uelewa wa vihatarishi vya maafa katika ngazi zote. | • Idadi ya tathmini za kina za hatari za maafa zilizofanywa katika ngazi zote.<br>• Idadi ya sekta zinazongatia taarifa za kina za hatari ya maafa katika utaratibu wa kuandaa mipango.<br>• Idadi ya mitaala ya usimamizi wa maafa na nyenzo za mafunzo zilizoandaliwa na kujumuishwa katika mfumo wa elimu ya juu na ufundi kwa kuzingatia ushahidi wa kisayansi unaotokana na tafiti za tathmini ya hatari ya maafa.<br>• Idadai ya tafiti za matuko za pamoja kati ya jamii, taasisi za utafiti na taasisi za elimu zilizohusika na usimamizi wa maafa zilinafanyika.<br>• Uwepo wa Jukwaa la utafiti na mtandao wa kushirikishana taarifa za usimamizi wa maafa.<br>• Idadi ya yaarifa za uhakika za wakati husika kuhusu usimamizi wa maafa kwa ajili ya wadau wote zililizotolewa.<br>• Taarifa ya utekelezaji wa Mikataba husika ya kikanda na kimataifa ya upatikanaji wa huduma za TEHAMA na taarifa za kijiografia.<br>• Tathmini zilizozingatia matumizi ya takwimu za picha za anga katika kupunguza hatari ya maafa.<br>• Uwepo wa mwongozo ya matumizi ya TEHAMA na huduma za kijiografia katika usimamizi wa maafa.<br>• Idadi ya kampeni ya uhamasishaji kuhusu hatari ya maafa zilizotekelezwa katika ngazi zote kwa kuzingatia uwezekano wa matukio ya maafa. | Uelewa wa hatari za maafa katika ngazi zote. |

| Malengo ya Kimkakati | Viashiria vya Matokeo | Matarajio/ Athari |
|---|---|---|
| | • Uwepo wa Mkakati wa uchechemuzi wa usimamizi wa maafa kuandaliwa na kufanya kampeni kwa watoa maamuzi kwa kuzingatia mwenendo wa matukio ya hatari za maafa katika sekta. | |
| II. Kuimarisha uwezo wa kuzuia, kupunguza madhara na kujiandaa na maafa katika ngazi zote kwa ajili ya ustahimilivu wa jamii. | • Idadi ya Miongozo ya namna ya kuzingatia masuala ya usimamizi wa maafa katika mipango ya maendeleo ya kisekta, mikakati, bajeti na programu katika ngazi zote iliyoandaliwa.<br>• Idadi ya mafunzo kwa sekta ya namna ya kuzingatia masuala ya usimamizi wa maafa katika mipango ya maendeleo.<br>• Asilimia ya ongezeko la matumizi ya bima katika usimamizi wa maafa.<br>• Idadi ya mafunzo na mazoezi ya vitendo ikiwemo majanga yanayovuka mipaka yaliyofanyika katika ngazi zote.<br>• Idadi ya mafunzo ya kuimarisha uwezo wa kutumia dhana ya afya moja yaliyotolewa katika ngazi zote.<br>• Idadai ya zana na programu za usimamizi wa magonjwa ya milipuko na wadudu wanaohama zilizoandaliwa, kuwianishwa na kutekelezwa.<br>• Idadi ya tamani zilizoandaliwaa na vituo vya kujihifadhi vilivyoanzishwa katika maeneo hatarishi kwa maafa.<br>• Idadai ya mafunzo ya uwezo wa kufanya tathmini ya uharibifu na mahitaji katika ngazi zote.<br>• Uwepo wa andiko la vigezo vya majenzi, kanuni na miongozo ya usalama lililoandaliwa au kurejewa.<br>• Taarifa ya mwenendo wa huduma za kinga za afya kwa magonjwa ya mlipuko. | Ustahimilivu wa jamii kuimarika. |

| Malengo ya Kimkakati | Viashiria vya Matokeo | Matarajio/ Athari |
|---|---|---|
| | • Asilimia ya ongezeko la miji na vijiji yenye mgawanyo na mipango ya usimamizi na matumizi ya ardhi.<br>• Idadi ya taarifa za mbinu bora za usimamizi wa maafa zilizotambuliwa na kushirikishwa kwa wadau.<br>• Idadi ya mikakati ya usimamizi wa maafa na mipango ya kujiandaa kukabiliana na maafa inayozingatia tathmini ya hatari za maafa za kisayansi inapowezekana iliyoandaliwa katika ngazi zote.<br>• Taarifa ya hali ya ongezeko la vifaa vya kisasa kwa taasisi zinazotoa huduma za utafutaji na uokoaji.<br>• Taarifa ya hali ya ongezeko na upatikanaji wa huduma za matibabu ya dharura katika ngazi ya mkoa. | |
| III. Kuboresha mifumo changamano ya tahadhari ya mapema ya majanga tofauti tofauti kwa kuzingatia mahitaji ya jamii. | • Taarifa ya maboresho ya mifumo na vifaa vya kisasa kwa taasisi zinazohusika na taadhari ya mapema na operesheni za dharura.<br>• Uwepo wa jukwaa la pamoja la kiteknolojia ya habari na mawasiliano la taarifa za usimamizi wa maafa na mfumo wa ubadilishanaji wa takwimu ili kusaidia taasisi zote zenye kuhusika na taadhari ya mapema lililounganishwa na Kituo cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura pamoja na uwepo wa utaratibu wa pamoja wa kutoa tahathari za mapema kwa umma.<br>• Uwepo wa mfumo wa matumizi ya TEHAMA na teknolojia ya taarifa za kijiografia katika utabiri, ufuatiliaji na usambazaji wa taarifa za tahadhari kwa umma na watu walio katika mazingira hatarishi kwa wakati na kwa njia inayotambulika kwa urahisi kwa jamii. | Uwepo wa mifumo changamano ya tahadhari ya mapema ya majanga tofauti tofauti inayozingatia mahitaji ya jamii. |

| Malengo ya Kimkakati | Viashiria vya Matokeo | Matarajio/ Athari |
|---|---|---|
| | • Idadi ya tafiti za maarifa ya jadi zilizorasimishwa katika tahathari ya mapema ya majanga tofauti tofauti.<br>• Uwepo wa taratibu za kawaida za uendeshaji na hadidu za utoaji wa taarifa za taadhari ya mapema.<br>• Uwepo wa ujumbe wa tahadhari ya mapema unaozingatia mahitaji ya mtumiaji wa mwisho ili kutoa mwelekeo wa hatua za kuchukua kwa makundi yaliyolegwa kupitia mifumo ya habari (radio, runinga, mitandao ya kijamii, magazeti, n.k.,) kwa majanga ya aina mbalimbali. | |
| IV. Kuimarisha uwezo wa kukabiliana na maafa na utoaji wa huduma za kibinadamu katika ngazi zote. | • Idadi ya timu za kukabiliana na maafa zinazojumuisha Wataalam kutoka sekta mbalimbali katika ngazi ya Taifa, Mikoa na wilaya zilizoanzishwa.<br>• Idadi ya mipango ya dharura ya taifa na kisekta iliyoandaliwa na kutekelezwa kwa kuzingatia ufahamu wa vihatarishi.<br>• Uwepo wa Mwongozo wa viwango vya msingi kwa ajili ya kutoa huduma za kibinadamu.<br>• Idadi ya Miongozo na taratibu za uratibu wa kukabiliana na maafa yanayovuka mipaka iliyoandaliwa.<br>• Kiasi cha bajeti na idadi ya vifaa katika maghala ya kimkakati na mpango wa kuhifadhi iliyotekelezwa kwa kuzingatia mwenendo wa matukio ya maafa.<br>• Taarifa ya ufuatiliaji na orodha ya uwezo wa kukabiliana na maafa katika ngazi zote.<br>• Uwepo wa mwongozo na huduma ya lishe na usaidizi unaohitajika kwa jamii wakati wa dharura na maafa. | Kuimarika kwa uwezo wa kukabiliana na maafa na utoaji wa huduma za kibinadamu katika ngazi zote. |

| Malengo ya Kimkakati | Viashiria vya Matokeo | Matarajio/ Athari |
|---|---|---|
| V. Kuongeza uwezo wa kurejesha hali, kukarabati na kujenga upya kwa ubora zaidi kwa ajili ya ustahimilivu wa jamii. | • Uwepo wa Miongozo na viwango vya kurejesha hali baada ya maafa (kukarabati na kujenga upya).<br>• Uwepo wa Miongozo ya kuzingatia hatari ya maafa katika kurejesha hali (kurabati na kujenga upya) katika sekta.<br>• Kiwango cha rasilimali za kufanya tathmini baada ya maafa.<br>• Mipango ya usimamizi wa maafa iliyorejewa na kujumjuisha masuala ya kujifunza kutokana na matukio yaliyopita.<br>• Taarifa ya hali ya utoaji wa usaidizi wa kisaikolojia na huduma ya afya ya akili na urekebishaji kwa watu wakati wa dharura na wakati wa hatua za kurejesha hali.<br>• Uwepo wa miongozo ya utoaji wa huduma za hifadhi ya jamii kwa makundi yaliyopo katika mazingira hatarishi ikiwa ni pamoja na uhamilishaji wa fedha pale inapowezekana kwa ajili ya kurejesha hali.<br>• Idadi ya tathmini ya mahitaji baada ya maafa makubwa zilizofanyika.<br>• Uwepo wa Mwongozo wa utafutaji wa rasilimali za kurejesha hali.<br>• Uwepo wa Mfumo wa Taifa wa Kurejesha Hali. | Ustahimilivu wa jamii kuimarika kupitia hatua za kurejesha hali, kukarabati na kujenga upya kwa ubora zaidi. |
| VI. Kuongeza upatikanaji wa rasilimali na uwekezaji katika usimamizi wa maafa kwenye sekta ya umma na binafsi. | • Andiko la mkakati wa utafutaji rasilimali na mfumo wa taifa wa uwekezaji katika usimamizi wa maafa.<br>• Andiko la mfumo wa uendeshaji wa ufadhili wa hatari za maafa, bima na ulinzi wa kifedha katika uwekezaji wa umma na binafsi kulingana na ukokotoaji wa makadirio ya madhara. | Kuongezeka mwitikio wa kutenga rasilimali na uwekezaji katika usimamizi wa maafa kwenye sekta ya umma na binafsi. |

| Malengo ya Kimkakati | Viashiria vya Matokeo | Matarajio/ Athari |
|---|---|---|
| | • Idadi ya mitandao ya usalama wa kijamii na Voluntia iliyoimarishwa ili kuleta ufanisi wa usimamizi wa maafa.<br>• Mwongozo wa utaratibu wa motisha ili kuhamasisha uwekezaji katika usimamizi wa maafa. | |
| VII. Kuimarisha mifumo ya utendaji ya usimamizi wa maafa katika ngazi zote. | • Idadi ya kanuni, taratibu na miongozo ya uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa maafa.<br>• Taarifs ya namna masuala ya usimamizi wa maafa yalivyojumuishwa katika mpango wa kitaifa na mwongozo wa bajeti kwa ajili ya kuzingatiwa katika sekta zote.<br>• Taarifa ya ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa na vifaa utendaji.<br>• Taarifa iliyofikiwa kurejea Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Maafa ya 2004.<br>• Andiko la Programu za kujenga uwezo wa mfumo wa usimamizi wa maafa na taarifa za utekelezaji.<br>• Idadi ya kamati za usimamizi wa maafa zilizojengewa uwezo katika ngazi zote.<br>• Uwepo wa ushirika wa sekta binafsi katika masuala ya usimamizi wa maafa.<br>• Andiko la Mfumo wa kitaifa wa matumizi ya TEHAMA katika usimamizi wa maafa. | Mifumo dhabiti ya utendaji ya usimamizi wa maafa katika ngazi zote. |
| VIII. Kuimarisha mchangamano wa jinsia, vijana, watu wenye ulemavu na mahitaji ya makundi | • Uwepo wa Mwongozo wa kuzingatia vipaumbele na ushiriki wa watu wenye ulemavu na makundi maalum mengineyo katika usimamizi wa maafa.<br>• Idadi ya programu maalum kwa ajili ya kujenga uwezo kuhusu usalama na | Shughuli za usimamizi wa maafa zinazozingatia mchangamano wa jinsia, vijana, watu wenye ulemavu |

| Malengo ya Kimkakati | Viashiria vya Matokeo | Matarajio/ Athari |
|---|---|---|
| maalum mengineyo pamoja na utofauti wa tamaduni katika usimamizi wa maafa. | • ustahimilivu kwa makundi maalum zilizoandaliwa na kutekelezwa.<br>• Mwongozo wa kuzingatia mahitaji ya jinsia, vijana, watu wenye ulemavu na makundi maalum mengineyo katika sera ya usimamazini wa maafa, program na miongozo ya uendeshaji.<br>• Taarifa ya hali ya ujumuishaji wa mahitaji ya makundi maalum ikiwemo wakimbizi na watu waliohama makazi katika awamu zote za usimamizi wa maafa.<br>• Taarifa ya hali ya kuzingatiwa utofauti wa tamaduni katika masuala ya usimamizi wa maafa. | na mahitaji ya makundi maalum mengineyo pamoja na utofauti wa tamaduni. |
| IX. Kuimarisha utekelezaji wa maazimio ya kikanda na kimataifa ambayo yameridhiwa | • Idadi na taarifa za utekelezaji wa makubaliano na mikataba baina ya nchi mbili, kikanda na kimataifa katika nyanja zote za usimamizi wa maafa.<br>• Idadi na taarifa za ushiriki katika mikutano ya kikanda na kimataifa, mafunzo, semina na mazoezi ya usimamizi wa maafa.<br>• Taarifa ya ushiriki katika mipango ya kukuza ushirikiano kikanda na kimataifa ya usimamizi wa maafa na huduma za kibinadamu.<br>• Taarifa ya hali ya uwepo wa mifumo ya kitaifa, kikanda na kimataifa ya gharama nafuu na matumizi rahisi pamoja na huduma ya kubadilishana taarifa kuhusu utendaji mzuri katika usimamizi wa maafa na huduma za kibinadamu.<br>• Taarifa kuhusu ushirikiano wa kikanda na kimataifa kwa taasisi za tafiti za kitaaluma na kisayansi na mitandao ya usimamizi wa maafa.<br>• Taarifa ya utekelezaji wa mifumo ya ufuatiliaji wa kiwango cha utekelezaji wa makubaliano na mikataba ya pande mbili, kikanda na kimataifa katika nyanja zote za usimamizi wa maafa. | Kuimarika kwa ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika masuala ya usimamizi wa maafa. |

| Malengo ya Kimkakati | Viashiria vya Matokeo | Matarajio/ Athari |
|---|---|---|
| X. Kuimarisha mbinu shirikishi za kisekta katika kudhibiti uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa ajili ya kuhimili maafa. | • Taarifa ya hatua za kujumuisha masuala ya usimamizi wa maafa katika mabadiliko ya tabianchi, uhifadhi wa mazingira na maendeleo endelevu.<br>• Mwongozo wa kuzingatia mfumo wa ekolojia na mazingira kuzingatiwa katika kufanya tathmini ya hatari ya maafa kitaifa.<br>• Taarifa ya mifano mizuri ya uwekezaji katika miundombinu ya buluu na kijani inayochangia katika kuimarisha ustahimilivu wa maafa.<br>• Idadi ya taarifa zilizozingatia mchangamano wa usimamizi wa maafa katika tathmini ya athari za mazingira na mapendekezo.<br>• Taarifa ya hali ya matumizi ya teknolojia na uvumbuzi kwa ajili ya kudhibiti mabadiliko ya tabianchi yanayohusiana na hatari za maafa.<br>• Taarifa ya utekelezaji wa programu ya kubadilishana uzoefu wa Sera na Mfumo wa pamoja wa usimamizi wa maafa na uhimili wa mabadiliko ya tabianchi. | Wadau wa maafa kuzingatia mbinu shirikishi za kisekta katika kudhibiti uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa ajili ya kuhimili maafa. |

## 7.7 Utaratibu wa kutoa taarifa na maoni

Mtiririko wa utoaji wa taarifa katika utekelezaji wa mkakati huu utafuata mfumo uliowekwa na Serikali wa kutoa taarifa. Mtiririko wa taarifa unaanzia kwenye vikundi vya watu, Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa kupitia kamati katika ngazi husika. Taarifa kutoka Sekretarieti za Mikoa, Wizara na Taasisi za umma zinazojitegemea zitaunganishwa na kuwasilishwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Ofisi ya Waziri Mkuu itaunganisha taarifa kutoka ngazi zote za utekelezaji wa shughuli mbalimbali ili kutoa taarifa jumuishi ya utekelezaji kwa robo mwaka, nusu mwaka na mwaka. Taarifa hizi zitashirikishwa kwa wadau wa usimamizi wa maafa kwa ajili

ya mapitio, majadiliano, kupanga upya na utekelezaji. Utaratibu wa kutoa maoni unatoa fursa ya mawasiliano ya kubadilishana taarifa kutoka pande mbili kati ya watayarishaji wa taarifa na watumiaji wa mwisho.

.

African Union. (2015). Agenda 2063: The Africa We Want. Framework Document. Addis Ababa: AUC. [online]. Available at: https://au.int/agenda2063/priorities

African Union. (2016). Programme of Action for the Implementation of the Sendai Framework for Disaster Risk Reduction 2015-2030 in Africa: In line with African Regional Strategy for Disaster Risk Reduction. [online]. Available at: https://www.preventionweb.net/files/67054_poaimplementationofthesendaiframewo[1].pdf

Ardhi University. (2001). Vulnerability Assessment Report. Prime Minister's Office. Dar es Salaam.

Ardhi University. (2003). Vulnerability Assessment Report. Prime Minister's Office. Dar es Salaam.

Ardhi University. (2008). Disaster Risks and Capacity Needs for Tanzania Mainland. Disaster Management Training Centre. Dar es Salaam.

Benson, C. (2009), Mainstreaming of Disaster Risk Reduction into Development: Challenges and Experience in the Philippines. ProVention Consortium.

Bündnis Entwicklung Hilft and IHFV (2019). World Risk Report 2019. *Focus: Water Supply*. [online]. Available at: https://reliefweb.int/sites/reliefweb.int/files/resources/WorldRiskReport-2019_Online_english.pdf

Climate & Development Knowledge Network (2014). *The IPCC's Fifth Assessment Report: What's in it for Africa?* Available at https://cdkn.org/wp-content/uploads/2014/04/AR5_IPCC_Whats_in_it_for_Africa.pdf

EM-DAT: The International Disaster Database – CRED. D. Guha-Sapir, Université Catholique de Louvain (UCL), Brussels. [online]. Available at: http://www.emdat.be. Accessed on 05 October, 2019.

Global Earthquake Model. (2018). Country Profile: Tanzania. [online]. Available at: https://downloads.openquake.org/countryprofiles/

INFORM. (2019). Tanzania Risk Profile. [online]. Available at: https://drmkc.jrc.ec.europa.eu/inform-index/Countries/Country-Profile-Map#

Msangi, C. E. (2016). Economic implications of natural disasters: the case of 2011 and 2014 floods in Dar es Salaam. Dar es Salaam. Ardhi University (*A Dissertation Submitted in Partial Fulfilment of the Requirements for the Degree of Master of Disaster Risk Management of Ardhi University*).

Örtengren, K. (2003). *Logical framework approach - a summary of the theory behind the LFA method*. Stockholm: Sida.

PMO, UNDRR and CIMA (2019). United Republic of Tanzania Disaster Risk Profile: Flood and Drought. [online]. Available at: https://www.undrr.org/publication/disaster-risk-profile-tanzania

Poggi, V., Durrheim, R., Mavonga Tuluka, G., Weatherill, G., Gee, R., Pagani, M., Nyblade, A., Delvaux, D. (2017). Assessing Seismic Hazard of the East African Rift: a pilot study from GEM and AfricaArray. Bulletin of Earthquake Engineering. Volume 15, Issue 11, 4499–4529, DOI: 10.1007/s10518-017-0152-4. [online]. Available at: https://maps.meteor-project.org/map/eq-pga-tza/#6/-6.137/35.701.

Schulz, K., Gustafsson, I., & Illes, E. (2005). *Manual for capacity development*. Stockholm: Sida.

UNDRR (2020), Multiple benefits of DRR investments – Reducing Risk and Building Resilience against floods and droughts in (Country). Available at: https://www.undrr.org/publication/multiple-benefits-drr-investment

UNDRR. (2015). Sendai framework for disaster risk reduction 2015-2030. [online]. Available from: http://www.unisdr.org/files/43291_sendaiframeworkfordrren.pdf.

UNDRR. (2018). DesInventar disaster database. [online]. Available at: https://www.desinventar.net/DesInventar/profiletab.jsp?countrycode=tza&continue=y

UNDRR. (2019). Words into Action guidelines: Developing national

disaster risk reduction strategies. [online]. Available at: https://www.undrr.org/publication/words-action-guidelines-developing-national-disaster-risk-reduction-strategies

UNDRR. (2020). *Tanzania: Risk-sensitive Budget Review*. Available at: https://reliefweb.int/report/united-republic-tanzania/united-republic-tanzania-risk-sensitive-budget-review

United Nations University (UNU). (2019). World Risk Report. [online]. Available from: http://ehs.unu.edu/news/news/world-risk-report-2014.html#info.

United Nations. (2015). Paris Agreement on Climate Change. [online]. Available from: https://unfccc.int/files/essential_background/convention/application/pdf/english_paris_agreement.pdf

United Nations. (2015). The 2030 Agenda for Sustainable Development. [online]. Available at: https://sustainabledevelopment.un.org/content/documents/21252030%20Agenda%20for%20Sustainable%20Development%20web.pdf

United Nations. (2017). General Assembly: Report of the open-ended intergovernmental expert working group on indicators and terminology relating to disaster risk reduction. [online]. Available at: https://reliefweb.int/report/world/report-open-ended-intergovernmental-expert-working-group-indicators-and-terminology.

United Nations. (2017). The New Urban Agenda. [online]. Available at: http://habitat3.org/wp-content/uploads/NUA-English.pdf

United Republic of Tanzania (1990), *Disaster Relief Coordination Act No. 9 of 1990*. Government Printer. Dar es Salaam

United Republic of Tanzania (2004). Disaster Management Policy of 2004. Government Printer, Dar es Salaam.

United Republic of Tanzania (2012). Tanzania Disaster Communication Strategy (TDCS), Prime Minister's Office, Dar es Salaam.

United Republic of Tanzania (2012). Tanzania Emergency Preparedness and Response Plan (TEPRP), Prime Minister's Office, Dar es Salaam.

United Republic of Tanzania (2012). Tanzania Long Term Perspective Plan 2011/12 – 2025/26: The Roadmap to a Middle-Income Country. President's Office, Planning Commission. Dar es Salaam.

United Republic of Tanzania (2014). National Operational Guidelines for Disaster Management of 201, Prime Minister's Office, Dar es Salaam.

United Republic of Tanzania (2015), *The Disaster Management Act, 2015 No. 7.* Government Printer. Dar es Salaam.

United Republic of Tanzania. (2000). Tanzania Development Vision 2025. Planning Commission. Dar es Salaam

United Republic of Tanzania. (2016). Five Year National Development Plans. Ministry of Finance and Planning. Dar es Salaam

United Republic of Tanzania. (2017). *Disaster Management Regulations of 2017.* Government Printer. Dar es Salaam

United Republic of Tanzania. (2018). Tanzania National Nutrition Survey of 2018. [online]. Available at: https://www.tfnc.go.tz/uploads/files/Leaflet_Tanzania%20National%20Nutrition%20Survey%202018_Printed.pdf

UN-OCHA. (2016). World Humanitarian Summit: Commitments to Action. [online]. Available at: https://reliefweb.int/sites/reliefweb.int/files/resources/WHS%20Commitment%20to%20Action_8September2016.pdf

Winson, A., Smith, K., Jordan, C., Mee, K., Huyck, C., Silva, V., Paul, N., Wagle, S., Evans, W., Kombe, E., Maholi, I., Jimee, G., Dashwood, C., Ciurean, R., Boon, D., Sampson, C., Henshaw, P., Msangi, C., Petrarulo, L., and Pradhan, S. and the METEOR: *METEOR: A methodology for assessing the potential for multi-hazard impacts on building exposure in developing nations.* Available online at: https://meteor-project.org/